

**Aunty Ezekiel ajifungua mtoto wa pili**

UKURASA 20



**Flick ataka kiwango kwa Sane**

UKURASA 21

## MAISHA


NOVEMBA 29, 2020 Nipashe

Baba, Mama na Mwana *Jumapili*



Ukurasa 14

**Pilipili ya kupikwa**



Ukurasa 15

**MAISHA NI NYUMBA**

WASWAHILI husema, 'nyumbani ndipo moyo wa mtu ulipo.'



**HARUSI**

Ukurasa 12

Jumapili Novemba 29, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • No. 0580414

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US



**UREMBO WA KUCHA**

**Si kujidai tu, huongeza kujiamini**

Ukurasa 1

# Bunge latoa tamko hatima kina Mdee

• **Lasema** linasubiri taarifa rasmi toka CHADEMA, BAWACHA 'yakandamiza', mwanasheria anena sheria ikifuatwa...

*Endelea ukurasa 2*



ESTER BULAYA

HALIMA MDEE

ESTHER MATIKO

SALOME MAKAMBA

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

**WAKAMATWA MADAI YA KUHUJUMU RELI**

## Mbaroni tuhuma kukutwa na vipande 10 meno ya tembo

UKURASA 3

# Kabudi ataka wasomi kupambana na propaganda za kuichafua nchi

UKURASA 3



Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play

App Store

**MICHEZO** YANGA INA JAMBO LAKE MSIMU HUU UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

## Wakamatwa madai ya kuhujumu reli

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

WATU saba wamekamatwa kwa tuhuma za uhujumu uchumi, baada ya kudaiwa kuhusika kuharibu miundombinu ya reli na kusafirisha mataruma kama chuma chakavu.

Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI), Robert Boaz, alisema watu hao wamekamatwa baada ya polisi kupata taarifa za watuhumiwa hao wakisafirisha vyuma chakavu vikiwamo vilivyoibiwa kutoka katika miundombinu ya reli.

Boazi alisema awali walikamatwa watuhumiwa watatu, baadaye ulifanyika uchunguzi na watuhumiwa wengine walikamatwa, wote wamefikishwa mahakamani kwa tuhuma za uhujumu uchumi.

Alisema watuhumiwa hao miongoni mwao wapo waliokuwa na mzigo, mawakala na wafanyabiashara wenye viwanda vya kuchakata vyuma chakavu.

Boaz aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Shakayai Gambarata, Shadrack Makulu, Halid Juma, Florence Mwebezi, Satyam Gupta, Luo Xingour na Rospick Kimaro.

Watuhumiwa hao walisomewa mashitaka yao na katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Pwani, mjini hapa mbele ya Hakimu Joyce Mushi.




Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Idd Kimanta (wa tatu kulia) na Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Kenani Kihongosi (wa pili kulia), wakiongoza matembezi ya kuhamasisha uchangiaji damu salama mkoani humo jana. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Bunge latoa tamko hatima kina Mdee

**Na Romana Mallya**

WAKATI Kamati Kuu ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), ikiwavua uwanachama wanachama wake 19, Bunge limeibuka na kusema linakisubiri chama hicho kupeleka taarifa rasmi.

Limesema hadi sasa (jana), bado Bunge linawatambua wabunge hao kwa sababu halijapokea taarifa yoyote inayoonyesha kuwavua uanachama.

Wabunge hao ni Halima Mdee, Grace Tendega, Esther Matiko, Cecilia Peresso, Esther Bulaya, Jesca Kishoa, Hawa Mwaifunga, Tunza Malapo, Naghenjwa Kaboyoka, Sophia Mwakagenda, Kunti Majala.

Wengine ni Anatropia Theonest, Salome Makamba Conchesta Rwamlaza, Angesta Kaiza, Nusrat Hanje, Asia Mohamed, Felister Njau na Stela Fiyao.

Juzi, Kamati Kuu ya CHADEMA ilikutana jijini Dar es Salaam chini ya Mwenyekiti wake, Freeman Mbowe, kuwajadili wabunge hao ambao waliapishwa Novemba 24, mwaka huu.

Hata hivyo, wabunge hao hawakujitokeza katika mahojiano hayo, lakini uamuzi uliofikiwa katika kikao hicho ni kuwavua uanachama na nafasi za uongozi ndani ya chama kwa madai ya kwenda kuapishwa pasipo kupata baraka za chama.

Akizungumza na Nipashe jana kuhusu hatima ya wabunge hao, Katibu wa Bunge, Stephen Kagaigai, alisema: "Mbunge yeyote bila kujali ni wa jimbo au Viti Maalum akiapa ni mbunge."

Alipoulizwa kama kanuni za Bunge zitaendelea kuwatambua wabunge hao baada ya CHADEMA kuwavua uanachama, Kagaigai alisema mpaka sasa Bunge bado linawatambua kuwa wabunge halali kwa sababu ofisi yake bado haijapata taarifa rasmi kutoka ndani ya chama chao.

Kagaigai alisema ofisi ya Bunge bado haijapata taarifa rasmi ya kuvuliwa uanachama wabunge hao, kwamba wakipewa taarifa watajua nini cha kufanya.

Nipashe ilimtafuta Dk. Ntengeki Nshala ili kufafanua kuhusu suala hilo ambalo limeleta mkanganyiko katika jamii. Dk. Nshala, ambaye ni mwanasheria, alisema endapo sheria na kanuni za Bunge zikifuatwa, wabunge hao hawatakuwa na sifa za kuendelea kuwa wabunge kwa sababu wameshavuliwa uanachama.

Hata hivyo, alisema endapo mambo mengine yatafuatwa nje ya sheria, wanaweza kuendelea kuwa wabunge wa viti maalum.

"Ukipoteza sifa ya uanachama huna haki ya kuwa mbunge. Kinachotakiwa kwa sasa ni taarifa zipelekwe bungeni na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kwa uamuzi uliofanywa na chama husika," alisema Dk. Nshala na kuongeza:

"Ila ukivuliwa uanachama una haki kama mtu mwingine kupinga na kudai haki yako mahakamani, wanachama hawa (wabunge) wanayohaki ya kufanya hivyo ama kwa kwenda mahakamani au kufuata utaratibu wa chama kuwasilisha malalamiko yao kama wanaona hawajatendewa haki," alisema Nshala.

Mbowe, akizungumza na waandishi wa habari juzi usiku, alisema wanachama hao wamekiuka katiba na kanuni za chama hicho, kwa uamuzi wao wa kwenda kuapishwa kuwa wabunge wa viti maalum bila ya kupitishwa na chama.

Mbowe alisema mbali na kuvuliwa uanachama wabunge hao, Kamati Kuu pia iliwavua nyadhifa walizokuwa nazo katika Baraza la Wanawake Chadema (BAWACHA), Baraza la Vijana Chadema (BAVICHA).

# ... BAWACHA 'yakandamiza' kufukuzwa kwao

**Na Enock Charles**

BARAZA la Wanawake Chadema (BAWACHA), limelaani kitendo kilichofanywa na baadhi ya viongozi wa chama hicho, kwenda kuapishwa bungeni bila kupata baraka za chama na kwamba wamevunja kanuni na taratibu za chama hicho.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam katika Makao Makuu ya chama hicho, Makamu Mwenyekiti wa BAWACHA Tanzania Bara, Sharifa Hamisi, alisema wamesikitishwa na kulaani kitendo hicho ambacho hakikutarajiwa na baraza hilo

"Tunafahamu wamekwenda huko kwa maslahi yao binafsi na si maslahi ya chama, msije kushawishiwa tena na wale eti mtapewa udiwani wa viti maalum. Binafsi nimesikitishwa sana na kitendo alichokifanya aliyekuwa Mwenyekiti wangu, Halima Mdee," alisema Hamisi.

Naye Mweka Hazina wa BAWACHA, Catherine Ruge, alisema pamoja na kazi kubwa iliyofanywa na wanachama hao waliofukuzwa, ambao baadhi yao walikuwa viongozi waandamizi wa baraza hilo, wamejishushia heshima yao na kufuta rekodi ya mazuri yote waliyofanya siku za nyuma ya kukijenga chama hicho.

"Waliamua kwa utashi wao kwenda kujiapisha bungeni bila kufuata utaratibu wa chama, bila kukiheshimu chama, nimeumia sana kwa sababu hawa watu tumefanya nao kazi kubwa sana ya kulijenga baraza letu," alisema Ruge.

Ruge alisema viongozi hao waliwajengea uwezo wa kujiamini wanawake, jambo ambalo lilisaidia katika kuwaonyesha fursa wanawake wa chama hicho.

Mmoja ya wajumbe wa Kamati Kuu CHADEMA, Suzan Kiwanga, aliwaomba wanachama wa BAVICHA kuwa watulivu katika kipindi hiki ambacho chama kinapitia katika wakati mgumu.

Kiwanga ambaye aliwahi kuwa Mbunge wa Mlimba alisema: "Chama kilikuwa kama kimezimika baada ya Halima na kundi lake kuapa bungeni. Lakini jana tumekiamsha upya. Mtu hawezi kuwa maarufu kuliko chama".

# Kabudi ataka wasomi kupambana na propaganda za kuichafua nchi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, amewataka wasomi kuiunga mkono serikali kupambana na propaganda za kuichafua nchi katika medani ya kimataifa.

Katika hotuba iliyosomwa kwa niaba yake na Mkurugenzi wa Siasa, Ulinzi na Usalama wa Wizara hiyo, Balozi Steven Hundi, wakati wa mafahali ya 23 ya Chuo cha Diplomasia (CFR) jijini Dar es Salaam jana, Prof.

Kabudi alisema wasomi wanao wajibu wa kusaidia kukabiliana na propaganda za kuichafua Tanzania katika uga wa kimataifa zinazofanywa na watu wasioitakia mema.

Bila kutaja majina ya aliowalenga, mtaalamu huyo wa sheria alisema wako watu wanashiriki kueneza propaganda zenye lengo la kuichafua taswira ya Tanzania kimataifa na kuharibu uchumi wa nchi.

Alisema wahitimu wa chuo hicho mahususi kwa masuala ya kidiplomasia na wasomi wengine nchini, wanao wajibu wa kulinda hadhi ya nchi kwa kushiriki kuwakabili watu wanaoendekeza propaganda hizo.

"Taifa letu liko katika ukombozi mkubwa wa kiuchumi lakini wakati huo huo tuko katika vita laini isiyohitaji silaha kuikabili vita vya kiuchumi. Katika nyakati hizi tunahitaji vijana wasomi kutetea nchi yetu.

"Hadi sasa, watu binafsi na sekta binafsi imeshiriki na kutoa mchango mkubwa katika uchumi wa nchi yetu. Hata hivyo, wasomi ni lazima waungane na serikali kupambana na watu wanaoleta propaganda za kuiharibu taswira ya nchi yetu kimataifa na kuharibu pia uchumi wetu.

"Kwa bahati nzuri, Tanzania tuna Rais ambaye anapambana kuwaletea wananchi maendeleo. Hii ndiyo diplomasia ya uchumi tunayopaswa kujivunia," alisema.

Katika hotuba yake hiyo, Prof. Kabudi pia aligusia Sera ya Mambo ya Nje ya Tanzania, akisema kwa sasa wamejikita katika kusaka wawekezaji kutoka nje ya nchi, kukuza utalii na biashara pamoja na kutafuta masoko ya kimataifa kwa bidhaa za Tanzania.

Alisema Tanzania pia imeendelea kushirikiana na jumuiya za kimataifa katika utatuzi wa migogoro, akisisitiza kuwa nchi inaendelea na msimamo wake wa kutofungamana na upande wowote.

Prof. Kabudi pia alikipongeza chuo hicho kwa kupanua huduma zake kwa kuanzisha matawi mapya katika mikoa mbalimbali nchini sambamba na kuanzisha kozi mipya ikiwamo ya ulinzi wa amani na utatuzi wa migogoro.

Aliuagiza uongozi wa chuo hicho kuweka nguvu kubwa katika matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), kukuza lugha ya Kiswahili, utafiti na machapisho ya kitaaluma ili kiwe na wahitimu ambao watakuwa washauri kwa wizara na serikali badala ya kuwa walalamikaji.

Wahitimu 679 walitunukiwa cheti cha kawaida, cheti cha ufundi, stashahada ya kawaida, stashahada ya juu, shahada na stashahada za juu za uzamili katika menejimenti uhusiano wa kimataifa, diplomasia ya uchumi na ulinzi amani na utatuzi wa migogoro kwa mwaka wa masomo 2019/20.

## RC ahimiza migodi kuwekeza miradi mikubwa ya kiuchumi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Mkoa wa Geita, Robert Gabriel, ameitaka migodi mikubwa ya uchimbaji madini mkoani Shinyanga, kuwekeza kwenye miradi mikubwa ya kiuchumi, ambayo itaubadilisha mkoa huo kimaendeleo.

Gabriel alisema hayo jana alipokuwa akitembelea mabanda ya uchimbaji madini ya almasi na dhahabu, kwenye uzinduzi wa Maonyesho ya Biashara na Teknolojia ya madini mkoani Shinyanga.

Alisema Shinyanga ina utajiri mkubwa wa madini, lakini maendeleo yake hayaendani na utajiri huo, hivyo kuitaka migodi mikubwa kuwekeza kwenye miradi mikubwa ya kiuchumi ili kuuwezesha kuendana na hadhi ya rasilimali ilizo nazo.

"Naiomba sana migodi mikubwa ya madini mkoani Shinyanga, muwekeze kwenye miradi mikubwa ya kiuchumi na kuacha alama siyo kuacha mashimo na umaskini. Mmechukua mali nyingi sana nyie na huu ni wakati wetu Watanzania kunufaika na rasilimali zetu," alisema Gabriel.

"Kipindi hiki cha awamu ya pili cha Rais John Mafuguli, hakuna kulala ni kubanana mpaka kieleweke. Achieni pesa muwekeze miradi mikubwa ya kiuchumi hata kama mkiondoka muache alama," aliongeza.



Mkuu wa Mkoa wa Geita, Mhandisi Robert Gabirel (kulia), akipata maelezo alipotembelea mabanda mbalimbali, baada ya kuzindua maonyesho ya biashara na teknolojia ya madini, mjini Shinyanga jana. Wengine ni Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack (wa pili kulia) na wa tatu kulia ni Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko. **PICHA: MARCO MADUHU**

## Mbaroni tuhuma za kukutwa na vipande 10 meno ya tembo

**Na Mary Mosha,** MOSHI

JESHI la Polisi mkoani Kilimanjaro linawashikilia watu wawili kwa tuhuma za kukutwa na vipande 10 vya meno ya tembo. Kamanda wa Polisi mkoani hapa, Emmanuel Lukula, alisema jana kuwa watu hao walikamatwa kutokana na taarifa za siri zilizotolewa na wananchi katika Kijiji cha Kikelelwa, Tarakea wilayani Rombo.

"Tulipokea taarifa kutoka kwa raia wema, tukazifanyia kazi na kuwakamata Nicholaus Kimaro (58) na Chrispin Tarimo (56), wakiwa na vipande 10 vya meno ya tembo, yenye uzito wa kilogram 23 yakipelekwa nchi jirani," alisema.

"Jeshi la Polisi halitawafumbia macho watu wanaocheza rasilimali za taifa na tutahakikisha tunawakamata na hatua kali za kisheria zinachukuliwa dhidi yao," aliongeza. Wakati huo huo, Kamanda Lukula alisema polisi wamewakamata watu sita wakiwa na kilo 482.78 za dawa ya kulevya aina ya mirungi na pikipiki 16. Alisema watuhumiwa hao wengi wao ni vijana, hivyo kuwataka kuacha tabia ya kujiingiza katika vitendo hivyo.


**KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPKI**

**ALEX FREDRICK TARIMO** anatangaza kupotelewa na kadi za pikpiki, **BAJAJ BOXER** yenye jina la **MOHAMED ENTERPRISES (T)LTD** namba za usajili **MC 646 CHH.**Chassis No. **MD2A21BY2KWC95204,**Engine **No.PFZWKC47881,BAJAJ BOXER** yenye jina la **LUKA HAULE BARAKA** namba za usajili **MC 781 CCY,**Chassis **No.MD2A21BY3JWH88064,**Engine **No.PFZWJH77348.**Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Taarifa ya polisi: DOD /DOD/RB/809246/2020.**



**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MOSHI DISTRICT REGISTRY**
**AT MOSHI**

**PC CIVIL APPEAL NO.18 OF 2020**

**ATANASIA ADOLPH KANJE.......................................APPLICANT**
**VERSUS**
**KIKUNDI CHA KUSAIDIANA**
**MBOMAI & TWO OTHERS..............................1ST RESPONDENT**
**JOSEPH PROSPER MASSAWE.......................2ND RESPONDENT**
**HAPPY JOSEPH KANJE .................................3RD RESPONDENT**

**TO: KIKUNDI CHA KUSAIDIANA MBOMAI**
**AND**
**JOSEPH PROSPER KANJE ,**
**WHERE VER YOU ARE.**

**NOTICE FOR MENTION**

**TAKE NOTICE:** That the above case has been fixed for mention in the High Court Of Tanzania at Moshi on 30th NOVEMBER , 2020 at 09:00am before Honourable T.MWENEMPAZI -J

WHEREAS: Service on you has been ordered to be published in the Nipashe newspaper.

You may appear in person or by Advocate or agent dully authorized to appear on your behalf and you are directed to produce on that day all the document upon which you intend to rely upon in support of your case.

TAKE FURTHER NOTICE THAT: In default of your appearance on that day and time the court may proceed in your absence.

GIVEN UNDER my hand and seal of the Court , this 27th day of NOVEMBER ,2020

O.H KINGWELE
Deputy Registrar
MOSHI

116015902



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA**
**MAHALI DODOMA**

**MAOMBI MADOGO NA.... YA 2020**

**BAINA YA LAURENT THOBIAS MASSAWE.............................MUOMBAJI**

**DHIDI YA**

**WADAIWA**
**BEST GROUP(T)LIMITED**
**EMMANUEL SAMSON MSYANI**
**CRDB BANK PLC**
**MCHINGA AUCTION MART AND REAL AGENCY CO.LTD**
**JAMES MOSES MARWA**

**KWA: BEST GROUP (T) LIMITED**
**EMMANUEL SAMSON MSYANI**
**CRDB BANK PLC**
**MCHINGA AUCTION MART AND REAL AGENCY CO.LTD**
**JAMES MOSES MARWA**

**POPOTE WALIPO**
**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya Maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili.

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria kataik Baraza hili wewe binafsi,Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 30.11.2020 saa 3.00 asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.

**ANGALIZO:** Kama haukuhudhuria tarehe iliyotwa hapo juu,Baraza likithibitisha kuwa umepokea Hati ya Wito, Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.

Hati hii imetolew kwa Amri yangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 27 mwezi wa Novemba, 2020.

MWENYEKITI,
DODOMA.

116019602

## DC awaonya 'mafataki' wanaorubuni wanafunzi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, amewaonya wanaume wilayani humo, kucha tabia ya kufanya mapenzi na wanafunzi.

Amesema kitendo hicho kinasababisha kuzima ndoto za wanafunzi, kwa kuwapatia ujauzito na kuacha masomo, pamoja na kuwaweka katika hatari zaidi ya kupata maambukizi ya virusi vya UKIMWI (VVU).

Mboneko aliyasema hayo jana wakati wa maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani, kilele chake kikitarajiwa kufanyika Desemba Mosi, mwaka huu.

Alisema wanaume kufanya mapenzi na wanafunzi ni kosa kisheria, kwa sababu watoto hao hawana uelewa katika matumizi ya kinga.

"Nawaonya wanaume acheni kutongoza wanafunzi, waacheni wasome ili watimize ndoto zao, mtawaharibia maisha kwa kuwapa ujauzito," alisema Mboneko.

Aidha, aliwataka wananchi kutowanyanyapaa watu ambao wanaishi na maambukizi ya VVU, bali washirikiane nao kufanya shughuli za kiuchumi.

Pia aliwataka watu wanaoishi na VVU kuendelea kutumia dawa za kufubaza makali, pamoja na wahudumu wa afya kuendelea kuwapatia huduma stahiki kwa wakati.

Kaimu Mganga Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Dk. Damas Nyansira, akisoma taarifa ya hali ya maambukizi ya VVU wilyani humo alisema yapo asilimia tatu, huku mkoa yakifikia asilimia 5.8.

# Gwajima awafariji waathirika volcano

**Na Edwin Mhagama**

MBUNGE wa Kawe, Josephat Gwajima, amewataka wakazi wa Kunduchi Mtongani ambao nyumba zao zimeathirika na tope la volcano kuwa watulivu, wakati serikali ikiendelea kutafuta namna ya kuwasaidia.

Alitoa kauli hiyo jana jijini Dar es Salaam wakati akikagua makazi ya wananchi yaliyoathirika na tope la volcano eneo la Kunduchi Mtongani.

Akiwa eneo hilo, Gwanjima aliwataka wananchi hao kutoa ushirikiano kwa serikali ikiwamo kufuata maelekezo yanayotolewa ili kuepuka madhara ambayo yanaweza kutokea baadaye.

"Kuwahamishia watu mahali lazima tujue watalala wapi, watakula nini, ukimpa mtu kiwanja bado hujamsaidia, tusikilize kwanza maelezo ya serikali halafu mimi kama mbunge nitashirikiana na nyinyi, bila shaka ndani ya wiki hii, ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, itasema neno," alisema Gwajima.

Aidha, Gwajima aliahidi kuwa katika hatua yoyote ambayo itachukuliwa na serikali, atahakikisha kila mwananchi anapata haki kutokana na tathmini itakayokuwa imechukuliwa.

"Nawapa pole sana kwa tukio hili ambalo limewapata, kama mwananchi mwenzenu na mwakilishi wenu nitafuatilia jambo hili kwa ukaribu sana, hakuna nyumba wala mtu ambaye ataonewa au kupunjwa kwa namna yoyote ile," alisema Gwajima.

Mmoja wa wakazi wa eneo hilo, Salome Mwapili, alisema tatizo la kutokea volcano katika eneo hilo lilianza miaka mitano iliyopita, kwamba lilianza kama kichuguu cha kawaida kabla ya kutoa ufa, kupasuka na baadaye kuanza kutoa kokoto, kisha matope mazito.

"Mvua ikinyesha, maji yanaingia ndani sababu ya hili tope maji yanakosa mahali pakwenda, lakini pia kuna chemchem isiyoisha, kwakweli hali siyo nzuri kama unavyoona," alisema Mwapili.

Mkazi mwingine wa eneo hilo, Rashidi Aboubakar alisema kutokana na athari hizo, shughuli nyingi za maendeleo zimesimama ikiwamo ujenzi, pamoja na huduma ya za kijamii.

Novemba 22, mwaka huu, Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam, Aboubakar kunenge, alitembelea eneo la Kunduchi Mtongani ili kutathmini athari zilizojitokeza, kwamba aliwataka wakazi hao kuhama ili kuepuka madhara ambayo yanaweza kutokea, kuahidi kuwa serikali itagawa viwanja vipya eneo lingine.




Mbunge wa Jimbo la Muheza, mkoani Tanga, Hamisi Mwinjuma 'Mwana FA' (wa pili kulia), akikabidhi funguo ya pikipiki kwa kijana, Elisha Paul, jimboni humo juzi, ambapo jumla ya pikipiki 23 zimetolewa kwa mkopo wa asilimia 10 kwa makundi ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Muheza. Kulia ni Mkuu wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani wa wilaya hiyo, Richard Muwe na (kushoto) ni Ofisa Maendeleo ya Jamii wilaya, Vije Mfaume. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Uwanja CCM Kirumba wageuzwa danguro usiku

**Na Richard Makore,** MWANZA

UWANJA wa mpira wa CCM Kirumba uliopo jijini Mwanza umegeuzwa kuwa danguro linalotumiwa na wadada wanaojiuza nyakati za usiku, maarufu kama machangudoa.

Uchunguzi uliofanywa na Nipashe umebaini kuwa eneo la nje la uwanja huo ambalo limejengwa flemu za biashara mbalimbali ambazo hazina wapangaji ndizo zinazotumika kwenye vitendo hivyo.

Baadhi ya wadada hao waliozungumza na Nipashe walisema kuwa pindi wanapopata wateja ambao hawana pesa ya kwenda nyumba ya wageni, wanazitumia flemu hizo kumaliza shida zao.

Aidha, uchunguzi wa Nipashe umebaini pia wadada hao wanajiuza kati ya Sh. 5,000 hadi 7,000.

Walilieleza Nipashe kuwa sehemu kubwa ya uwanja huo kwa nje nyakati za usiku hauna taa zinazomulika, hivyo inawapa urahisi wao kufanikisha shughuli zao kwenye giza.Mmoja wadada hao aliyejitambulisha kwa jina moja la Angela alisema analazimika kufanya kazi hiyo ili kujikimu kimaisha, ingawa familia zao hazijui.

Alisema ana miaka 18, anaishi na wadogo zake wawili, kwamba anapoondoka nyumbani nyakati za jioni wanajua anafanya kazi kwenye baa na siyo kujiuza.

Alisema ili kazi yao iweze kufanyika vizuri wameajiri mlinzi ambaye wanamlipa Sh. 1,000 kila wanapopata mwanamume na kungia naye katika flemu hizo.

Aliongeza kuwa mlinzi huyo ndiye anayelinda baadhi ya flemu zilizozunguka uwanja huo.

Mdada mwingine anayefanya kazi ya kujiuza, aliyejitambulisha kwa jina la Rose Ntika, alisema idadi yao kwa siku inaweza kufikia 80 hadi 100 kutegemea siku ilivyo.

Aliongeza kuwa siku za mwisho wa wiki idadi hiyo huongezeka kwa kuwa kuna biashara zaidi, ikilinganishwa na siku za kati kati ya wiki.

Mlinzi wa eneo hilo, ambaye alijitaja kwa jina la Dominic Mwita, alisema fedha anazokusanya kutoka kwa machangudoa hao Sh. 1,000 ni kwa ajili ya kuwapatia ulinzi wasidhurike na baadhi ya wateja wakorofi.

Nipashe lilimtafuta Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Mwanza, Julius Peter kuelezeka hali hiyo, alisema hana taarifa za uwanja wao kutumika kama danguro.

Hata hivyo, alisema atafuatilia suala hilo kwa kuwa linafanyika usiku kwa kificho nyakati za usiku. Aliongeza kuwa kama ni kweli watachukua hatua ili kulinda heshima ya chama na uwanja huo, ambao hutumiwa kwa ajili mpira na mikutano mbalimbali ya serikali na chama.

Nipashe pia ilimtafuta Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mwanza, Muliro Jumanne, ambaye alisema suala hilo linakuwa gumu linapopelekwa mahakamani.

Alisema ili kukomesha biashara hiyo inatakiwa wateja wa machangudoa hao ambao ni wanaume wakamatwe.

Kamanda Muliro alisema hakuna ushahidi unaojitosheleza pale machangudoa hao wanapofikishwa mahakamani.

## HABARI KITAIFA



Katibu Tawala Mkoa wa Morogoro, Mhandisi Emmanuel Kalobelo, akijaribu kuwasha moja ya pikipiki 18, zilizotolewa na Ofisi ya Bonde la Wami/Ruvu kupitia mradi wa uendelezaji sekta ya maji awamu ya pili, kwa viongozi wa Jumuiya za Watumiaji Maji mkoani humo juzi, ili kuboresha usimamizi na ufatiliaji wa vyanzo vya maji. Wa tatu kushoto ni Mkurugenzi wa bonde hilo, Simon Ngonyani akishuhudia makabidhiano hayo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Dk. Mpango ahimiza kilimo cha mkakati

**Na Mwandishi Wetu,** KIGOMA

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, amewataka wakazi wa Mkoa wa Kigoma kujishughulisha na kilimo cha mazao ya kimkakati na kutumia vyema soko la ndani na nchi jirani ya Burundi.

Dk. Mpango ambaye pia ni Mbunge wa Buhigwe, alitoa rai hiyo alipotembelea Kata za Kilelema, Muyama na Kasumo, wilayani Buhigwe, kuhamasisha shughuli za maendeleo na kuwashukuru wananchi kwa kumchagua Dk. John Magufuli kuwa Rais wa Tanzania na yeye kuwa mbunge kwa kura za kishindo.

Aliwataka wananchi hao kujihusisha na kilimo cha mazao ya kimkakati ikiwamo kilimo cha parachichi, mawese, tangawizi, mboga na matunda na kwamba serikali itapeleka mbegu za kisasa ili kuwa na uzalishaji wa mazao wenye tija.

Pia aliwahimiza kuhakikisha wanalinda amani, usalama na utulivu wa nchi kwa nguvu zote ili wananchi waendelee kujiletea maendeleo yao katika nyanja mbalimbali za kiuchumi.

Dk. Mpango aliwaahidi wananchi hao kutekeleza ahadi alizotoa wakati wa kampeni kwenye sekta ya elimu, maji, afya, nishati, ujenzi wa miundombinu ya barabara pamoja na kuendeleza kilimo ndani ya miaka 5 ijayo.

Akimkaribisha kuzungumza na wananchi hao, Mkuu wa Wilaya ya Buhigwe, Kanali Michael Ngayalina, alimwomba Waziri Mpango kusaidia kutatua changamoto mbalimbali zinazoikabili wilaya zikiwamo maji, barabara, soko la kimataifa na elimu.

Kanali Ngayalina alieleza mikakati mbalimbali iliyopo ya kukabiliana na changamoto ya maji kwamba serikali inatekeleza mradi wa maji wenye thamani ya Sh. bilioni 2.8 utakaopita katika vijiji vya Migongo na Kilelema.

Mkakati mwingine ni ujenzi wa daraja la Mto Malagarasi litakaloiunganisha wilaya na nchi jirani ya Burundi, ikiwa ni sehemu ya mradi wa ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kutoka Kabingo mpaka Manyovu.

Katika ziara yake, Dk. Mpango ametembelea Kata nane kati ya 20 zilizoko kwenye Buhigwe. Kata hizo ni Munanila, Mwayaya, Munzeze, Janda, Bukuba, Kilelema, Muyama na Kasumo.

# Mongela ataka nguvu itumike dhidi ya wabakaji

**Na Richard Makore,** MWANZA

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, John Mongela, ameliagiza Jeshi la Polisi mkoani humo kutumia nguvu katika kupambana na watu wanaofanya vitendo vya ukatili wa kijinsia, ikiwamo kuwabaka watoto na kuwapa mimba.

Mongela alisema hayo jana wakati wa maadhimisho ya siku 16 za kupinga ukatili wa jinsia, yaliyofanyika jijini hapa na kuhudhuriwa na wadau mbalimbali.

Alisema mikoa ya Kanda ya Ziwa ina takwimu za juu kuhusu vitendo vya ukatili dhidi ya watoto na wanawake, kwamba nguvu za ziada zinahitajika kupambana navyo.

Mkuu huyo wa mkoa aliitaka jamii kufichua vitendo vya ukatili wa kijinsia badala ya kuvifumbia macho, kwa kuwa vinaathiri maisha ya watu wanaofanyiwa hivyo.

Kutokana na hali hiyo, alimwagiza Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Muliro Jumanne, kusimamia suala hilo, ili kulikomesha na kwamba ikiwezekana wawapoteze wabakaji.

Alisema juhudi za kupambana na vitendo hivyo zinarudishwa nyuma kutokana na badhi ya wazazi ambao wanakubali kupokea zawadi kutoka kwa wahalifu ili wamalize kesi nje ya mahakama.Kamanda Muliro aliahidi kutumia nguvu kupambana na watu hao kama wanavyofanya katika mapambano dhidi ya majambazi.

"Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa agizo lako tutalitekeleza kwa nguvu nyingi bila uoga ili kukomesha ukatili wa kijisnia kwenye jamii," alisema Kamanda Muliro.

Naye Mkuu wa Dawati la Jinsia la Polisi mkoani Mwanza, Faraja Mkinga, alisema mwaka huu matukio 1,387 yameripotiwa.

Aliongeza kuwa kesi 455 zilifikishwa mahakamani ingawa baadhi ya watu waliofanyiwa ukatili wa kijinsia wanashindwa kutoa ushirikiano kwa kutoa ushahidi.

Mkurugenzi wa Shirika la Kivulini ambalo linatoa msaada kwa watoto wanaofanyiwa ukatili, Yassin Ally, alisema vitendo hivyo bado vinaisumbua jamii.

# DC awa mbogo watumishi waliokimbia vituo

**Na Ambrose Wantaigwa,** RORYA

MKUU wa Wilaya ya Rorya, Simon Odunga, ameagiza watumishi wa Halmashauri ya Wilaya hiyo wanaoishi nje ya wilaya, kuhamia katika vituo vyao kazi ndani ya siku 90.

Alisema tangu halmashauri ilipoanzishwa, kuna baadhi ya watumishi wameendelea kuishi nje ya wilaya hiyo, wakisafiri umbali mrefu kufika katika vituo vyao vya kazi.

Odunga alitoa agizo hilo juzi wakati akikagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kusikiliza kero za wananchi. Alisema lengo la serikali ya awamu ya tano ni kuhakikisha wananchi wanapata huduma za msingi kama vile afya, elimu na maji kwa wakati, huku nidhamu ya watumishi wa umma ikipewa kipaumbele.

Pia alishangazwa na uamuzi wa baadhi ya watumishi wa wilaya hiyo kuendelea kuishi wilaya jirani ya Tarime, baadhi yao wakichelewa kazini bila ya sababu za msingi.

Kadhalika, alihimiza Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kuwekeza katika ujenzi wa nyumba bora wilayani hapa, kutokana na kuwapo kwa upungufu mkubwa baada ya kuanzishwa wilaya hiyo iliyomegwa kutoka Tarime.

Naye Mbunge wa Rorya, Jaffari Chege, alisema tayari ofisi yake iliwasilisha mapendekezo katika ofisi ya Mkurugenzi Mkuu wa NHC juu ya kuwekeza katika jimbo hilo ambalo idadi ya wakazi wake iliongezeka baada ya kuanzishwa Wilaya ya Rorya.

"Ofisi yangu iliwasiliana na Mkurugenzi wa NHC kuelezea umuhimu wa kuwekeza katika sekta ya majengo bora kutokana na mahitaji makubwa yaliyopo jimboni hapa," alisema Chege.

Alisema watumishi wote wa umma bila kujali vyeo wahakikishe wanaepuka kufanyakazi kwa mazoea, kujenga utaratibu wa kutembelea wananchi maeneo yao pamoja na kutatua kero.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hatua zichukuliwe kukomesha rushwa ya ngono vyuo vikuu

**SUALA** la rushwa ya ngono katika taasisi za elimu ya juu, limekuwa likilalamikiwa na watu mbalimbali huku ikielezwa kuwa linazidi kuwa sugu mwaka hadi mwaka.

Kabla ya kuanza kusemwa kwa uwazi, vitendo hivyo vilikuwa vikifichwa huku baadhi ya watendewa wakiogopa kujitokeza ama kwa kuhofia kufukuzwa kazi kwa watumishi au kukatishwa masomo kwa wanafunzi.

Vitendo hivyo, kwa mujibu wa taarifa mbalimbali, vimekuwa vikifanywa na baadhi ya wanataaluma (maprofesa na wahadhiri) dhidi ya wanafunzi kwa lengo la kuwafaulisha kwenye masomo yao. Kwa wafanyakazi, vimekuwa vikidaiwa kufanywa na mabosi dhidi ya watumishi wa ngazi za chini kwa nia ya kuwafanyia upendeleo katika masuala mbalimbali ikiwamo kupandishwa vyeo.

Katika miaka ya 2000, suala hilo lilianza kuwekwa wazi huku baadhi ya wahusika wakitajwa kupitia vyombo vya habari ikiwamo mitandao ya kijamii, hatua ambayo ilisababisha baadhi ya taasisi zilianza kuwachukulia hatua watuhumiwa.

Mwaka jana na mwaka huu, hatua kali zaidi zilianza kuchukuliwa dhidi ya wahusika baada ya kuelezwa kuwa vinazidi kuota mizizi na hata kuzifanya baadhi ya taasisi ambazo watumishi wake wanaodaiwa kujihusisha kuanza kutajwa na kutishia kuporomoka.

Uongozi wa baadhi ya vyuo hivyo, ulianza kuwachukulia hatua ikiwamo kuwafukuza kazi baada ya kufikishwa katika ngazi mbalimbali za kinidhamu na ushahidi kwa wazi kupatikana.

Taarifa hizo pia zilitikisa katika jamii baada ya kudaiwa kuwa vitendo kama hivyo vinafanyika katika Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustine (SAUT) jijini Mwanza. Hatua hiyo iliufanya uongozi wa chuo kuibuka na kukiri kuwapo na kubainisha kuwa umeanza kuchukua hatua.

Matokeo ya utafiti yaliyotolewa juzi, yamebainisha kushamiri kwa vitendo hivyo kwenye vyuo vikuu na taasisi mbalimbali za elimu ya juu. Taarifa hiyo ya utafiti uliofanywa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na mfuko wa Wanawake Tanzania (WFT), ilivitaja UDOM na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) ambacho ni kikongwe nchini kuliko vyote, kuwa ni vinara wa vitendo hivyo.

Taarifa hiyo imebainisha wazi kuwa vitendo hivyo si tu vinazidi kushika kasi bali vinaharibu taswira ya Tanzania katika elimu ya juu ikiwamo kutiliwa shaka kwa wahitimu ambao ni tegemeo kubwa katika ujenzi wa taifa.

Kutokana na kukithiri kwa vitendo hivyo, ni vyema hatua zaidi zikachukuliwa katika kupambana na watu ambao wanajihusisha katika kuichafua nchi. Serikali itoke na tamko katika kupambana na vitendo hivyo ambavyo havina lengo jema na mustakabali wa taifa.

Kama wahenga wasemavyo mzaha mzaha hutumbuka usaha, madhara ya vitendo hivyo ni makubwa iwapo hatua hazitachukuliwa. Ni vyema hatua zikachukuliwa mapema kabla ya janga kuwa kubwa zaidi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Kaulimbiu siku ya UKIMWI iwe chachu ya kubadili tabia

**MAADHIMISHO** ya Siku ya UKIMWI Duniani, yatafikia kilele keshokutwa, yakiwa na kaulimbui isemayo; 'Mshikamano wa Kimataifa, Tuwajibike kwa Pamoja'.

Kwa sasa makongamano mbalimbali yakiwamo ya kisayansi kwa ajili ya kujadili mwelekezo wa udhibiti wa VVU na uchangishaji wa fedha za Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI (ATF) vinaendelea.

Mwaka huu maadhimisho ya Siku ya UKIMWI Duniani kitaifa, yanatarajiwa kufanyika Moshi mkoani Kilimanjaro, huku mgeni rasmi akitarajiwa kuwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa.

Makongamano yanaendelea kufanyika huku kukiwa na taarifa kuwa zaidi ya asilimia 50 ya maambukizo mapya ya virusi vya UKIMWI nchini yapo kwa kundi la vijana wenye umri wa kati ya miaka 15 hadi 35.

Hiyo ni kwa mujibu wa Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Uratibu na Uwekezaji, Dorothy Mwaluko, kwamba maambukizo mapya nchini bado ni tishio, hivyo kuna haja ya kutekeleza mikakati yote ya kuhakikisha yanatoweka.

Katibu Mkuu huyo anasema takwimu zinaonyesha kuwa takriban watu 72,000 wanapata maambukizi mapya kwa mwaka, na kwamba hiyo ina maana kuwa kwa mwezi ni watu 6,000.

Katika hesabu hizo, anasema kwa siku ni watu 200 wanaoambukizwa na kwa saa moja ni watu wanane, hivyo anashauri mikakati itekelezwe kwa namna mbili ili kukabiliana na hali hiyo.

Mkakati wa kwanza anautaja kuwa ni kwa kundi lililoambukizwa virusi hivyo na kuendelea kufanya kazi, kwa kuwa mtaji wa maskini ni nguvu na sio virusi na wa pili ni kuweka mikakati ili wale wasioambukizwa wasiambukizwe.

Ni kweli kwamba ili vijana wasiambukizwe ni muhimu waongozwe watambue kuwa miili yao ndiyo maisha yao na pia maisha yao ndiyo nguvu ya ujenzi wa taifa lao, hivyo ni vyema waepuke UKIMWI.

Wakati huu wa kuelekea kwenye kilele cha maadhimisho ya siku hiyo, ni vyema kutafakari kwa kina na kutafuta njia ya kuwaokoa vijana kwenye janga hilo kubwa linalopotengeza nguvu kazi ya taifa. Kwa kuwa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 hadi 2025 inalezea jinsi ambavyo serikali imejipanga kukabiliana na ugonjwa huo kwa kipindi cha miaka mitano ijayo, basi ni vyema mikakati hiyo ikatekelezwa.

Ukisoma ukurasa wa 140 wa ilani hiyo, CCM inasema, miaka mitano ijayo itaendelea kuisimamia serikali ili kuendeleza mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI kwa kuzingatia mikakati iliyoainishwa katika Mkakati wa Nne wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI (NMSF IV 2018/19 - 2022/23).

Mkakati huo unatajwa kuwa ni kuendeleza mikakati ya kudhibiti maambukizo mapya ya virusi vya UKIMWI, ikwamo maambukizo ya mama kwenda kwa mtoto, kifua kikuu, ukoma na homa ya ini.

Inaahidi kuandaa mkakati endelevu wa kifedha ili kuimarisha mfuko wa udhamini wa kudhibiti UKIMWI Tanzania, ili kuwahudumia vyema waathirika, kupunguza kasi ya maambukizo mapya katika jamii kwa kuimarisha mikakati ya kupunguza maambukizo mapya kwa watoto na makundi maalum.

Makundi hayo ni yale ambayo yapo katika mazingira hatarishi zaidi ya kuambukiza na kuambukizwa virusi vya UKIMWI, kuongeza programu zenye ubunifu zinazozingatia umri na jinsia.

Programu hizo zitajikita zaidi katika kushughulikia utambuzi wa hatari za maambukizo ya VVU na mikakati ya kupunguza madhara kwa kutumia nadharia sahihi za kubadili tabia.

Vijana nao wana wajibu wa kuzingatia kile kinachoelezwa kwa ajili ya kufanikisha vita hiyo dhidi ya UKWIMI, ambao kwa miaka mingi tangu mwanzoni mwa miaka ya 80 unaendelea kutesa watu duniani.

Kundi hilo halina budi kutambua na kujilinda dhidi ya UKIMWI kwa kuepuka ngono zembe, kususia ngono, na hasa kuwa waaminifu, kwa kuwa virusi vinaweza kusambazwa wakati wa ngono na hata kutoka kwa mama walioambukizwa hadi kwa watoto wachanga.

Vijana wanatajwa kama nguvu ya mabadiliko kwenye nyanja mbalimbali, hivyo nguvu zao hizo za mabadiliko wazitumie pia kubadili tabia na mienendo yao kwa ajili ya kujiepusha na maambukizi ya UKWIMWI.

Ni imani kwamba vijana wakiamua kubadilika ama kubadili tabia na mwenendo wao kwa ujumla, Tanzania bila UKWIMWI inawezekana.

SAFU

## FIKRA MBADALA



Nkwazi Mhango, Canada

# Tubadili mfumo wetu wa utumishi wa umma

PAMOJA kupata uhuru takriban miaka zaidi ya 60 iliyopita, nchi nyingi za kiafrika kama si zote zilisahau, au tuseme, makusudi, hazikubadili mifumo yake ya uendeshaji wa serikali zake.

Kimsingi, nchi hizi zilirithi mfumo wa kikoloni na kuendelea hata kuung'ang'ania kwa manufaa ya watu wachache wenye nguvu katika jamii. Kutokana na mfumo huu wa kikoloni na kinyonyaji, nchi zote za kiafrika zilibakia maskini pamoja na nyingi kujaliwa utajiri wa rasilimali.

Kuna msemo kuwa Afrika ina utajiri wa maliasili, lakini ikikaliwa na watu maskini hata kuliko wa nchi nyingi za Magharibi zisizo na rasilimali za kutosha ikilinganishwa na ilizojaliwa Afrika.

Katika safu ya leo, tutaangazia baadhi ya maeneo au mambo tunayopaswa kuyabidili haraka ili kuendelea na kuwawezesha wananchi wetu kufaidi utajiri mwingi waliojaliwa na Mungu. Yafuatayo ni mambo husika:

Ni bahati mbaya kuwa baadhi ya wazito wetu wanaosimamia rasilimali zetu wanaishi maisha sawa na yale ya waliowang'atua, kuwatimua na kuwarithi ama kwa makusudi au kwa kutojua ukichia mbali kunogewa na utamu wa hali na mifumo hii.

Ni hatari kuwa ni wachache wanaoliona na kulidurusu hili. Kutokana na mfumo huu zandiki, nchi za kiafrika zimekuwa zikipoteza fedha nyingi za walipa kodi kwa matumizi mabaya ya watu wachache badhirifu na fisadi. Ndiyo maana Rais John Pombe Magufuli alipoingia madarakani, alijaribu kuuteketeza mfumo huu pale alipofumua baadhi ya mambo kama vile ajira hewa, wanafunzi hewa na matumizi mabaya ya fedha na rasilimali za umma bila kusahau rushwa huku akianzisha ubanaji matumizi yaliyolenga kuwakomboa wanyonge.

Hii ndiyo siri ya Tanzania kupiga maendeleo haraka na kuweza kuwa kwenye kundi la nchi za kipato cha kati ndani ya miaka mitano; jambo ambalo halijawahi kufanywa na nchi yoyote.

Leo nitatoa baadhi ya mifano kuhusu namna Afrika inapaswa kuanza kuangalia upya mifumo yake ya uongozi na matumizi yasiyo ya lazima. Hivi, katika karne ya 21, kuna haja ya baadhi ya watendaji wetu kuwa na ma-bodyguard (walinzi) au madereva wakati hawana tishio lolote na kuwatumikia wananchi kama kweli wanawatumikia wananchi au kuweza kufanya kama vile kuendesha magari yao kwenda na kurudi kazini? Hapa Kanada, wazito wengi huendesha magari yao na hawana ma-bodyguard au madereva na kuwahudumia waliowachagua vilivyo.

Je, hawa wetu wanamuogopa nani kama kweli wanawahudumia mabosi wao ambao ni wale wanaowawakilisha? Je, ni fedha kiasi gani tunapoteza na ukale wa mfumo huu wa kikoloni? Wakoloni walihitaji madereva kwa vile hawakujua nchi zetu. Walihitaji ma-bodyguard kwa vile walikuwa wakitunyanyasa na kutunyonya. Ukiondoa viongozi wa kitaifa ambao wanahitaji ulinzi kama huu, hawa wadogo kama vile wakuu wa mikoa, wilaya na wengine wanahitaji kwa mfano madereva na wasaidizi wakati ni watumishi wa kawaida?

Hapa Kanada majaji, na wakuu wengine hujiendesha wenyewe. Chukulia mfano majaji. Kama wanahitaji madereva ili wasichoke, inakuwaje maprofesa wanaowaandaa hawa majaji au madaktari wanaookoa maisha ya watu wanajiendesha na hakuna kinachoharibika?

Kimsingi, wenzetu wa nchi za Magharibi walioanzisha mifumo fujaji na nyonyaji kwa makusudi mazima. Mfano, wakuu wa kila idara walilindwa kwa hofu ya kudhuriwa na wale waliokuwa wakiwatawala kimabavu na bila faida.

Hakika, tunapaswa kuanza kutoza kodi viongozi au watumishi wa umma wanaopata mishahara mikubwa na huduma za bure kama hizi za madereva na wasaidizi wasiohitajika. Ukiachia mbali watumishi wa umma, huku si rahisi kuwa na wasichana wa kazi kama ilivyo nyumbani. Hii ni kwa sababu hakuna mwenye uwezo wa kuwalipa mshahara wa kiwango cha chini ambao kila mmoja wa wafanyakazi wa kawaida analipwa. Hivyo, uwepo wa uwezekano wa kuajiri wasichana wa kazi ni njia mojawapo ya kinyonyaji ambayo inapaswa kuangaliwa sambamba na maslahi ya wakubwa yasiyo na faida wala ulazima kwa taifa.

Kwa vile Rais Magufuli anasifika kwa kubana matumizi, anapaswa kuanza kuangalia maeneo ya wasaidizi wake wa ngazi mbalimbali kuanzia wizara, mikoa, wilaya na idara.

Akifanya hivi, ataokoa mabilioni ya fedha ambayo yatamsaidia kufikia azma yake ya kuibadili Tanzania haraka iwezekanavyo.

Mwisho, hebu tujiulize. Ni fedha kiasi gani tunapoteza kama nchi na jamii kwa kuendekeza mfumo huu ambao waliouanzisha na kuacha walishaachana nao zamani na kujua madhara yake kwa watu wao na mataifa yao?

Wakoloni waliweka mfumo huu wa kinyonyaji na kivivu kwa vile walikuwa hawawatumikii wananchi bali kuwatumia na kuwanyonya kwa faida ya mataifa yaliyowatuma. Isitoshe, waliofaidi hizi huduma ni maofisa wa kikoloni tu na si wananchi.

Kama profesa au wakili anaweza kuendesha gari lake, inakuwaje vigumu kwa majaji kufanya hivyo?

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO



Na Joseph Kulangwa

# Sekta binafsi iwezeshwe kuokoa tasnia ya habari

HIVI karibuni akizungumza kwenye mkutano mkuu wa Shirikisho la Klabu za Waandishi wa Habari Tanzania (UTPC), Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk Hassan Abbasi, alitoa kauli nzuri na mwafaka kwa tasnia ya habari nchini.

Dk Abbasi ambaye pia ni Msemaji Mkuu wa Serikali, alizungumzia umuhimu wa wafanyakazi katika vyombo vya habari nchini, kuwa na mikataba ya kazi, ili kuleta mazingira ya usalama na haki kazini.

Kiongozi huyo alitoa kauli hiyo baada ya kuambiwa na washiriki wa mkutano huo wa siku mbili uliofanyika Morogoro Novemba 16 na 17, mwaka huu, jinsi hali halisi ilivyo katika baadhi ya vyombo vya habari.

Mgeni huyo rasmi, akasema ataiagiza Tume ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), kuhakikisha kwamba wafanyakazi katika vyombo vya elektroniki kwa maana na redio na televisheni, nao wanatekeleza matakwa hayo ya kiutumishi na kuweka mazingira mazuri ya kazi.

Ni kweli, kuwa mazingira ya kazi na maslahi katika vyombo vingi vya habari nchini, husussan vya binafsi ni duni, kutokana na kipato cha vyombo hivyo kupungua kwa sababu mbalimbali, lakini kubwa ikiwa ni ya matangazo.

Si siri, kwamba matangazo ndiyo roho ya kiuchumi ya chombo chochote cha habari, mbali na mauzo ya nakala, na katika redio na televisheni ni zaidi, kwa sababu bila matangazo, hakuna kipato hakuna malipo.

Kutokana na hali hiyo, baadhi ya wamiliki wamewageuza wafanyakazi wao katika vyumba vya habari kama vibarua au wa kujitolea. Imefika hata baadhi ya waandishi kuomba kujitolea na si kuajiriwa, kwa sababu hakuna ujira wa kuwalipa.

Matokeo yake, waandishi wamekuwa wakiishi kwa posho za nauli katika vikao wanavyoalikwa kuhudhuria kuchukua habari. Hali hiyo pia imechangia baadhi kukiuka maadili ya uanahabari na kupokea rushwa, ili kumsifia au kumchafua mtu au taasisi.

Wapo baadhi ya wamiliki kwa kudharau wafanyakazi wao, wamekuwa wakiwapanga mstari na kuwalipa chochote alichonacho mfukoni siku hiyo, kama nauli ya kuwaleta na kuwarudisha nyumbani. Mfanyakazi akihoji huambiwa hali ni mbaya.

Na kweli, kama hakuna tangazo linaloingia huku gharama za uendeshaji zikiongezeka, ni nini matarajio ya mwajiri? Ataishia tu kulipa kijungujiko na maisha kuendelea kuwa magumu kwa wafanyakazi wake.

Ingawa Dk Abbasi si Katibu Mkuu wa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi inayosimamia TCRA, ni dhahiri atawasiliana na mwenzake wa wizara husika, ili vyombo vyote vya habari viitekeleze hili.

Ni wazi sasa kwamba kutokana na hali hiyo, upo umuhimu wa vyombo hivi kuwa chini ya wizara moja, pengine ikaitwa Wizara ya Habari na Mawasiliano, ili vyombo kusimamiwa kwa pamoja na kuleta ufanisi.

Lakini pia, ipo haja kwa Serikali hasa kwa kuzingatia kauli ya Rais John Magufuli akizindua Bunge la 12 hivi karibuni, ya Serikali kushirikiana kwa karibu na sekta binafsi, kuelekeza taasisi za umma hata binafsi kupeleka matangazo yao kwenye vyombo hivyo kama ilivyokuwa awali.

Utaratibu wa Idara ya Habari, Maelezo, kusimamia matangazo kwenye vyombo vya habari, umeviathiri, kiasi kwamba kama hali hii itaendelea, kwa muda mfupi, ni wazi vitakufa na kubakiwa na mitandao ya kijamii katika kuhabarisha, kuelimisha na kuburudisha umma.

Wapo wanaoaimini kwamba nafasi ya magazeti, redio na televisheni katika jamii imekuwa finyu, kwa sababu leo taarifa ziko kiganjani kupitia mitandao ya kijamii, bila kujali uhakika na ukweli wa habari hizo ambazo hazifanyiwi kazi.

Ukweli ni kwamba hata kwa aina ya Bunge la 12 lilivyo, lenye idadi kubwa ya wabunge wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), watu wengi watategemea zaidi magazeti na redio, kujua mengi ya upande wa pili (Upinzani) kuliko wa CCM ambao una wasemaji wengi bungeni tayari.

Naiomba Serikali izingatie dhamira yake ya kushirikiana na sekta binafsi, ikiamini kwamba ndiyo yenye mchango mkubwa katika kutoa ajira kwa Watanzania, kwa kuwa ndiyo hasa inayotakiwa kufanya biashara na si Serikali. Alamsiki!

## KONA YA UKWELI



Na Thobias Mwanakatwe

# CHADEMA waacheni kina Mdee watumikie wananchi

NOVEMBA 24, 2020 bila shaka itawekwa katika kumbukumbu ya historia ya vyama vingi vya siasa.

Nasema itaweka kumbukumbu kwa sababu ni siku ambayo unaweza kusema kulifanyika kitu cha 'surprise' pale wabunge 19 wa Viti Maalum wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) walipoamua kwenda jijini Dodoma kuapishwa kuwa wabunge.

Wabunge hao walichukua uamuzi huo ambao uliacha maswali mengi si tu kwa viongozi na wanachama wa CHADEMA lakini pia kwa wananchi ambao wamekuwa wakifuatilia mwenendo wa siasa nchini tangu kufanyika kwa uchaguzi mkuu Oktoba 28, 2020.

Itakumbukwa Chadema na Chama cha ACT Wazalendo baada ya kutangazwa matokeo ya kura za urais, wabunge na madiwani viongozi wa vyama, hivyo walitoa msimamo wao wa kutokubali uchaguzi huo na kukataa katakata kupeleka majina ya wabunge wa viti maalum kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) ili wateuliwe kuwa wabunge kwa mujibu wa sheria.

Wakati wakitoa matamko hayo, wanawake ambao walishiriki mchakato wa kutafuta wabunge wa viti maalum ndani ya chama chao kumbe walikuwa na lao moyo kwa maana hawakukubaliana na uamuzi uliotangazwa na vyama vyao na ndio maana Novemba 24 wakaamua kupuuza matamko ya viongozi wao na kwenda kuapishwa Dodoma.

Kwanza, nachukua nafasi hii kuwapongeza wabunge wanawake wa CHADEMA kwani kitendo walichokifanya ni cha kizalendo sana ambacho kinapaswa kuungwa mkono na wananchi wapenda maendeleo na wanaolitakia mema taifa letu.

Taifa letu linawategemea sana hususani kinamama na sasa Halima Mdee na wenzako mkawe sauti ya wanawake wengine nchini ambao hawakupata nafasi ya kuwa viongozi lakini kupitia ninyi sauti zao zitasikika mkiwiwakilisha vyema katika changamoto zao zinazowakabili.

Halima Mdee, Ester Bulaya na Ester Matiko, lazima mtambue kuwa ninyi ni jeshi kubwa ambalo mlikusanya mabinti ambao waliamini kwamba ni viongozi bora na kutamani kuwa kama ninyi. Suala la kufukuzwa uanachama mtafute hali yenu katika vyombo vya sheria.

Tambueni kama msingekwenda kuapa na kuwa wabunge mngenyong'onyesha mioyo za mabinti kwa kufuata upepo tu wa kisiasa wa viongozi wenu wachache wenye chuki dhidi ya taifa letu la Tanzania.

Aliyepewa kapewa hilo hata vitabu vya dini limebainisha hakuna wa kuwanyang'anya isipokuwa mwenyezi Mungu.

Haikuwa na maana kususia maendeleo ya wananchi ambao wanawategemea mkawe sauti zao kisa vuguvugu la kisiasa la baadhi ya viongozi wenu wachache ambao hawana mapenzi mema na Tanzania.

Mlichokifanya kimedhihirisha yote mliyoyafanya katika kipindi cha kampeni mpaka uchaguzi mkuu yalikuwa ya haki usawa na uwazi, sasa hapa kazi tu.

Sote tunajenga nyumba moja ya nini kugombaniana fito, tuache propaganda na turudi kuwatumikia wananchi wasiokuwa na hatia ya chochote.

Nadhani sasa mtakuwa mumeshajionea njia sahihi ya kupita ni ipi badala ya kufuata upepo wa watu wanaowapoteza kwani kukosa kwao kusiwafanye na nyie mkose, nyie mumepewa hamna budi kupokea.

Katika hili la wabunge wa viti maalum Chadema, ACT Wazalendo Watanzania ambao ni wanachama na wapenzi au wafuasi wa vyama vya siasa nchini wana la kujifunza mpaka sasa.

Najua wabunge viti maalum mliokula kiapo mtasemwa maneno mengi na mtaitwa majina mengi lakini nachowaomba msikate tamaa, zibeni masikio kazi iendelee Watanzania wapenda maendeleo wako pamoja nanyi.

**MUNGU IBARIKI TANZANIA, MUNGU WABARIKI WABUNGE VITI MAALUM**

**Kwa maoni na ushauri tumia barua pepe mwanakatwe2015@gmail.com**

## DARASA LA NDOA



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka 0744000066

# Umuhimu wa urafiki na uchumba kwa ndoa bora

SAFARI ya ndoa huanza na uhusiano kwa wahusika kufahamiana. Kufahamiana kunaanza na urafiki. Si lazima kila mtu awe rafiki. Mtu anaweza kukupenda lakini si muhimu awe rafiki. Marafiki huchaguliwa.

Kuna matatizo mengi yanayotokea katika ndoa nyingi siku hizi. Uzoefu unaonyesha kuwa matatizo mengi yanayosababisha kuvunjika kwa ndoa nyingi yanatokana na sababu kuu tatu za ujumla:

Sababu hizo ni kukosekana kwa uamuzi makini wakati wa kutaka kuoa au kuolewa; malezi na makuzi mabaya wakati wa utoto, na kukosekana kwa ufahamu na maarifa ya kutosha kuhusu taasisi ya ndoa.

Maisha ni hatua. Vijana wengi wameingia katika ndoa bila kupitia hatua ya urafiki, kwa maneno mengine wamekuwa wachumba kisha kuoana bila kupitia hatua ya urafiki, hivyo kutokufahamiana vizuri. Maisha yenye mafanikio yanahitaji utaratibu, subira na uvumilivu.

Bahati mbaya, vijana wengi siku hizi wanakurupuka na kuingia katika ndoa na matokeo yake ni majuto.

Wako waliohusiana na watu ambao wamekuwa vikwazo katika maisha yao; wamefisha ndoto zao, malengo na maono yao; wameua imani katika Mungu na furaha yao.

Mada hii ya urafiki na uchumba inakusudia kuwasaidia vijana kujitambua ili kufanya uamuzi sahihi kwa wakati sahihi na kwa mtu sahihi.

**URAFIKI NI NINI?**

Kwa tafsiri ya kawaida, urafiki ni uhusiano mzuri kati ya watu wawili au zaidi. Mtu anaweza kuwa na marafiki zaidi ya mmoja na urafiki unaweza kudumu kwa miaka mingi.

Sababu kubwa za kuwapo urafiki ni kukidhi mahitaji ya kibinadamu ya kutambuliwa, upendo na mapenzi; ushirika; ushirikiano na umoja/mshikamano; kufahamiana; kufundishana na kuelekezana; na kupata mwenzi wa maisha.

Pamoja na kuwapo sababu za urafiki, kuna urafiki wa aina tofauti kama vile marafiki wa mbali. Hawa ni wale marafiki tunaokutana nao au kushirikiana nao katika mambo ya kawaida ya kila siku.

Pia kuna marafiki wa kawaida ambao tunapenda kuwa nao katika vitu tunavyopenda kuvifanya. Lakini pia wako marafiki wa karibu ambao tunapenda kuwashirikisha mambo yetu ya binafsi na kuwa nao katika matukio mbalimbali.

Licha ya aina hizo za marafiki, pia kuna marafiki wa karibu sana. Hawa ni wale tunaowaamini sana na kuwashirikisha siri zetu au mambo yetu ya ndani na muhimu sana. mara nyingi huwa si wengi, hawazidi watatu.

Aina nyingine ni rafiki wa moyoni. Huyu ni yule mmoja na wa pekee ambaye umempa moyo wako wote na maisha yako. Anaweza kuwa mpenzi, mchumba au mwanandoa.

Kadhalika yuko rafiki mshauri. Aina hii ya marafiki ni wale marafiki waliotutangulia kiumri, uzoefu au maarifa ya kimaisha. Ni urafiki unaojengwa katika misingi ya kulea na kufunza maarifa ya kimaisha na kiroho.

**EPUKA URAFIKI HUU**

Pamoja na kuwa na aina hizo za urafiki, si kila urafiki ni wa kuuzingatia, hivyo uko ule ambao mtuu kuuepuka. Urafiki huu ni ule unaojengwa katika misingi ya mali, fedha au vitu.

Mwingine ni ule unaotanguliza ngono ambao Mungu katelekezwa; unaojengwa katika misingi ya kutaka sifa; wa kulazimishwa; wenye misingi ya mihemko, matamanio na kupumbazwa. Aliyepumbazwa hashauriki. Pia si lazima kila mtu awe rafiki yako.

**MWENZI WA MAISHA**

Suala la kumpata mwenzi wa maisha si la kukurupuka wala kufanya pupa kwa sababu bila kulifanya kwa utulivu linaweza kugharimu maisha yako yote yaliyobaki.

Jambo la msingi, katika kutafuta mwenzi wa maisha unapaswa kumshirikisha Mungu haja ya moyo wake. Mtu anapaswa kumwomba Mungu amwonyeshe atakayemfaa, atakayemtubariki, kwani Mungu anapoamua kukubariki, hutoa mtu wa kutimiza kusudi lake.

Pia unapaswa kutengeneza marafiki kwani mchumba atatokana na marafiki ulionao. Thibitisha na eleza wazi hisia zako juu yake na pia omba ushauri kwa watu wanaokujua na wanaomjua.

Jambo lingine muhimu ni kushirikisha wazazi au walezi wako; kufahamu tabia zake, marafiki zake na familia anayotoka. Andaa utaratibu wa kukutana naye kwa mazungumzo na kufikia makubaliano.

Kama ilivyoelezwa awali kwamba vijana wa kizazi cha sasa kinakurupuka katika kupata wenzi ndiyo maana ndoa nyingi zinaingia matatani muda mfupi baada ya kufungwa.

Kutokana na hali hiyo, kijana anatakiwa asiwe na haraka. Mambo mazuri hayahitaji haraka.

Aidha, unapoanzisha urafiki na mtu yeyote kwa ajili ya maisha ya baadaye (ndoa), rasimisha uhusiano wako (officialise the relationship). Uchumba huanzia hapa.

**Itaendelea Jumapili ijayo**

● **Dk. Mlyuka ni Mchungaji wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare) inayojihusisha na masuala la Ndoa na Malezi ya Watoto. Kwa ushauri na maoni wasiliana naye kwa barua pepe: info@tamcare.or.tz**

# MAISHA

NOVEMBA 29, 2020
Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*






Ukurasa 14

## Pilipili ya kupikwa



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

WASWAHILI husema, 'nyumbani ndipo moyo wa mtu ulipo.'



## HARUSI

Ukurasa 12



### UREMBO WA KUCHA

## Si kujidai tu, huongeza kujiamini

Ukurasa 14

# ‘Hausigeli’ anapokataa kula, huharibu watoto pia

Na Moses Ismail



NI mzee wa makamu ya miaka 70 hivi, amevutiwa na mapengo ya mtoto mdogo msichana aliyekuwa ameongozana na dada mmoja, akaamua kumtania kwa kumuta: “Aaa, mapengooo!”

Kwa sauti ya ukali unaoonekana dhahiri, yule dada ambaye bado pia ni msichana mdogo mwenye kama miaka 19 hivi, akamwambia yule mtoto: “Mwambie koma, mapengo mama yako.”

Halikuwa jambo zuri kwa watu walioshuhudia, hasa tukiangalia umri wa yule mzee na maneno ya dada aliyeongozana na yule mtoto, lakini baya zaidi ni pale mtoto alipotii amri na kumwambia mzee wa watu: “Mapengo mama yako.”

Waliokosa uvumilivu kwa tukio hili lililotokea nje ya duka moja maeneo ya Bahari Beach, tukiwa tumejikinga mvua, wakaanza kumshambulia kwa maneno makali yule dada wakimshutumu. Hakujali, akabishana nao.

Ndipo mmoja kati yetu akauliza: “Hivi huyu ni mtoto wake?” Lakini mmoja kati yetu, anayemfahamu yule dada, akajibu kwa kusema: “Sio mtoto wake. Huyu ni mfanyakazi wa nyumba ile pale (akionyesha kwa kidole).”

Nikatafakari, mfanyakazi wa nyumbani anayemfundisha mtoto kujibu majibu mabaya kama kama haya tena mbele za watu, je, ameshamfundisha maneno mangapi mengine mabaya?

Achana na muonekano wa nyumba ya kifahari tuliyoonyeshwa kwamba ndipo wanapotoka dada na mtoto yule, zipo nyumba nyingi katika jamii zetu ambazo wenye nyumba huishi na madada wa nyumbani kama hawa.

Wanapoenda kazini, huwaacha watoto wao na madada hao ambao hukaa na watoto kwa muda mrefu zaidi kuliko wazazi wenyewe. Kwa maana hiyo watoto hujifunza mambo mengi toka kwa madada hao kuliko kwa wazazi wao.

Bahati mbaya kwa wazazi wengi ni kwamba, madada hawa wa nyumbani hawawafunzi watoto wala hawatamki maneno mabaya kama hayo na huwa makini katika kusimamia adabu na lugha ya mtoto awapo na wazazi wake.

Kwa maana hiyo, inachukua muda mrefu sana mzazi kujua iwapo kama mtoto wake anatumia lugha mbaya na za kukera na hilo hutokea tu pale mtoto atakaporopoka maneno hayo mbele zao.

Na linapotokea hilo, ni wazazi wachache wanaoweza kutulia na kujiuliza ni wapi mtoto wake alikojifunzia lugha hiyo ili hali anayesoma shule nzuri, anayekaa katika jamii iliyostaarabika na wala hachezi na ‘watoto wabaya’?

Badala yake wazazi wengi hukimbilia kuwachapa watoto hao huku wakiwalazimisha kusema “sema sirudii tena kusema hivyo” bila ya kumuuliza mtoto nani aliyemfundisha maneno makali kama hayo yanayofanya amchape.

La mtoto na dada wa Bahari Beach ni mfano wa tabia za baadhi ya madada wa nyumbani zinavyo haribu watoto ambazo ili mzazi hazifahamu, inabidi amdadisi mtoto wake kirafiki juu ya yale yanayotokea wakati wanapobaki peke yao na dada.

## NA HAMIS KIDAGO 0657 207168 QUIZ

**Oanisha maneno kutoka kifungu A na yale ya kifungu B kwa mujibu wa jinsi yanavyoendana (kijinsia).**

**A**


- Beau **D – Belle**
- Blanc **E – Blanche**
- Bon **I – Bonne**
- Faux **L – Fausse**
- Fous **J – Folle**
- Frais **N - Fraîche**
- Long **M – Longue**
- Nouveaux **A – Nouvelle**
- Roux **H – Rousse**
- Vieux **B – Vieille**
- Gentil **F – Gentille**
- Doux **K – Douce**
- Jaloux **C – Jalouse**
- Gros **G – Grosse**

**B**

- Nouvelle
- Vieille
- Jalouse
- Belle
- Blanche
- Gentille
- Grosse
- Rousse
- Bonne
- Folle
- Douce
- Fausse
- Longue
- Fraîche

## WATOTO

# PAKA RANGI



## CHEKA



Alichokifanya daktari

Kijana mmoja alikwenda sokoni kununua nyanya, hali ilikuwa hivi kati yake na muuzaji.

**Kijana:** Nyanya zinauzwa kiasi gani?

**Muuzaji:** Kilo shilingi 1500

**Kijana:** Lakini nataka unisagie nataka kwenda kula na chipsi nyumbani

**Muuzaji:** Kijana usitanie kazi za watu, kwenda hukoo

Swali

Matunda yana faida zipi kwa binadamu?

# MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



## Tafuta kulijua kusudi la kuumbwa mwanamume, mwanamke duniani

KARIBU tena msomaji katika mwendelezo wa makala zetu zinazojadili jinsi maisha yalivyo kila siku. Ndoa nyingi zimekuwa zikikumbwa na misukosuko inayosababisha mafarakano na hata zingine kuvunjika.

Yote hayo yanatokea kwa sababu lipo eneo muhimu ambalo wengi hawajalitilia maanani. Nalo ni kusudi la Mungu la kumuumbwa mwanaume na mwanamke katika ulimwengu huu. Usimuulize mwingine makusudi hayo ya uubaji bali muulize Mungu pekee. Na kimsingi, Mungu aliumba mume na mke si kuachana bali kuambatana.

Ni ukweli uliofichika ambao ni muhimu sana ufahamike ili ndoa nyingi zinazotikisika zipone. Mwanamume aliumbwa ili awe baba. Na neno baba lina maana tano.

Kwanza, baba ni chanzo au chimbuko na msingi wa familia ya mwanadamu kwani wote walitoka maungoni mwake. Huyu mwanamume alifinyangwa kwanza, ndipo mwanamke akafuata. Kinachotangulia kinajenga msingi, kisha vingine vinajengwa juu yake. Chochote afanyacho kinatizamwa kwa macho mawili. Mwanaume ndiye mkuu wa familia.

Mwanaume amebeba ukoo wote kiunoni mwake. Isitoshe, umuhimu wa mwanaume unatokana na majukumu yake. Anapaswa kuwa na hekima ya kuhudumia familia yake kwa ajili ya maisha ya baadaye. Aweke mazingira salama kiafya na kiuchumi hata pale atakapokuwa hayupo duniani.

Pili, baba ni mpaji. Ni mtu ampaye mwingine vitu (giver). Utunzaji wa familia unatokana na baba. Hata Mungu aliweka wazi katika moja ya maandiko yake pale aliposema, "Lakini ye yote asiyewatunza wale wa nyumbani mwake hasa, ameikana imani, tena ni mbaya kuliko mtu asiyeamini".

Tatu, baba ni mtengenezaji. Anao uwezo wa kutengenza familia/watoto. Ndio maana mwanamume hapaswi kuikimbia familia. Mwanamume anapokimbia familia yake kwa sababu yoyote ile, mwanamke hubaki anashangaa. Yeye ni nguzo, alimkaribisha mwanamke kwa kumuoa, anapomkimbia anaonekana ni kituko.

Watoto nao hushangaa wasipomuona baba yao ambaye ni kichwa cha familia. Walimzoea katika malezi. Mungu katika neno lake akasema, "Nanyi kinababa, msiwachokoze watoto wenu, bali waleeni katika adabu na maonyo ya Bwana. Hakuna katika familia kuwa mwanamke ni mleaji, popote panapotajwa malezi ni baba. Ukiona mwanamke analea, huyo ni mjane au hana mume.

Nne, Mwanamume ni kinga. Mwanamume ndiye anayepewa wajibu kutokana na kusudi aliloumbiwa yeye ni kinga. Ndiye anayepaswa kulinda uumbaji wa Mungu. Zaburi 11: neno linasema, "Kama misingi ikiharibika, mwenye haki atafanya nini?" Ndoa nyingi zinasambaratika kwa sababu ya chanzo ambaye ni mwanamume hasa pale anapokwepa majukumu yake.

Tano, mwanamume ni mtetezi. Ni mtu anayepigania haki za wengine. Asidhulumiwe yeyote alipo mwanamume.

Mpenzi msomaji, bila shaka umepata picha kusudi la kuumbwa mwanamume. Sasa tumgeukie mwanamke. Kusudi la kwanza, mwanamke ni msaidizi wa baba/mwanamume. Aliumbwa aweze kutoa msaada. Vitu vyote vya kumsaidia mwanamke Mungu aliviweka ndani ya mwanamume.

Ndio maana akasema kwenye neno lake, Mwanzo 2:18 "Si vema mtu huyu awe peke yake, nitamfanyia msaidizi wa kufanana naye". Mwanamume na mwanamke wakiishi bila kujua makusudi waliyoumbiwa na Mungu, watajikuta matatani wakati wote.

Pili, mwanamke hukuza na kuzidisha kile umpacho. Ukimpa neno, yeye anakupa maneno. Ukimpa wazo la mradi atahakikisha analipanyia kazi. Kila umpacho atakikuza, zidisha na kukurudishia kikiwa kimeongezeka. Mama kwa asili anazidisha na kukurudishia.

Ukishaanza kumpiga msaidizi wako, hiyo ni ishara ya kushindwa uongozi. Hii ni salamu kwa wale wanaopiga wake zao.

Tatu, Mungu ameweka uwezo mkubwa sana kwa mke amsaidie mwanamume na kumlinda. Katika ubongo wa mwanamke Mungu ameweka chumba cha ziada. Anamsikiliza mwanamume lakini moyoni hakipo

Nne, mwanamke mambo yote yameunganishwa pamoja. Analea na kufanya kazi zingine. Tano, mwanamke anao uwezo wa kushawishi na sita anao uwezo wa ujasiriamali. Kila akipatacho ni kwa ajili ya kusaidia.

Bila shaka msomaji wangu umepata kidogo kuelewa nini kusudi la Mungu kuwaumba wanaume na wanawake. Laiti wengi wetu tungesimama kwenye nafasi zetu na kuyatafakari makusudi hayo, mitikisiko kwenye ndoa nyingi isingekuwepo.

Tuishie hapa kwa leo. Tukutane tena wiki ijayo kwa neema ya Mungu tuendelee kuchimbua Maisha Yalivyo kila uchao. Ukiwa na maoni, ushauri au kisa chochote cha maisha, nitumie ujumbe mfupi kupitia ***0715268581.*** Namba hii pia ipo ***WhatsAPP.***

# NAWAZA KWA SAUTI

Na Salome Kitomari



## Ukombozi mwanamke ni wa jamii nzima, tuungane kutafuta suluhisho

MAADHIMISHO ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia yanaendelea na yatafika kilele Desemba 10, mwaka huu, chini ya kaulimbiu ya 'Maendeleo ya Wanawake ni Faida kwa Jamii Nzima'.

Katika kipindi hiki, asasi zisizo za kiserikali na wadau mbalimbali wanashirikiana kwa karibu kuwa na matukio yanayogusa maisha ya wanawake moja kwa moja, ikiwamo kutumia shuhuda za baadhi yao kwa ajili ya kuainua wengine.

Maadhimisho haya yanafanyika kukiwa bado kuna changamoto ya usawa wa kijinsia sehemu za kazi, ngazi ya jamii na katika fursa mbalimbali, bado mali zimetumika kundamiza haki za wengi.

Bado mila na tamaduni za baadhi ya maeneo zinamdunisha mwanamke na kumwona bado hawezi hadi awe na msaada wa mwanamume, bado kipaumbele cha ajira na masomo kipo kwa watoto wa kiume, bado urithi wa mali unaonekana ni halali zaidi kwa mwanamume kuliko mwanamke.

Kaulimbiu ya mwaka huu inatufungua macho kuwa ukimwendeleza, kumwinua au mwanamke akiendelea si kwa faida yake mwenyewe bali jamii yake kwa ujumla.

Inakuwa jamii kwa sababu mwanamke ndiye mlezi wa familia kwa maana kama atafanikiwa au kuwa na nguvu ya kiuchumi maana yake watoto wake watasoma na kuishi vizuri, atatunza kipato cha familia na kuhakikisha maendeleo yanakuwapo.

Kutokana na wengi wa wanawake kukuzwa katika mfumo kandamizi, wengi wamejikuta katika maumivu mengi na makubwa licha ya kuwepo mifumo inayolinda haki zao.

Bado wanawake wanapigwa, wanajeruhiwa, wanadhulumiwa, wanatelekezwa kwa sababu ambazo hazina mashiko yoyote kwamba mwanamke amekosa basi anapigwa, kujeruhiwa na kuuwawa na inapokuwa kinyume chake hakuna hatua inayochukuliwa.

Ni lazima ubinadamu uwepo katika jambo lolote, kwamba unampiga huyu kwa sababu hajafanya moja mbili, lakini nawe usipifanya maana yake naye akupige.

Ziko jamii mtoto wa kike haruhusiwi kusoma, bali anasubiriwa akishakuwa anakuwa mali ya mwanamume, jambo ambalo limetengeneza utegemezi kwa kiasi kikubwa.

> **"Maadhimisho haya yawe chachu ya kuleta mabadiliko makubwa ya kifikra na ukombozi dhidi ya mwanamke ambaye naye ataikomboa jamii yake kipato chake kitaisaidia jamii.**

Ni lazima jamii iunge mkono jitihada za kumnyanyua mwanamke na kupinga ukatili ambao umfichwa kwenye kivuli cha mila na desturi ambazo kimsingi nyingine hazina maana.

Mathalani, mila ya kulazimisha mtoto aolewe haina maana kwa kuwa mtoto anapaswa kuwa shuleni, asaidiwe kufikia ndoto zake na si vinginevyo.

Bado hajawa na misuli ya kumudu majukumu ya kindoa ni lazima asomeshwe na kufundishwa kuwa na nguvu ya kiuchumi ambayo itamwezesha kuishi maisha mazuri pasipo kunyanyaswa na aliye na nguvu kiuchumi.

Ipo mifano mingi ya wanawake ambao wanaonyesha njia kuwa mafanikio ya wanawake ni ya jamii nzima na kutokana na mchango wao mkubwa kwa jamii wamefanikiwa kuleta mabadiliko makubwa ambayo ni kwa faida ya jamii.

Wapo wanawake waliowahi na wapo kuwa katika ngazi za juu za uamuzi hawakupewa hizo nafasi bali walitafuta na kuomba kazi kutokana na sifa zao ambazo zilitokana na wao kusoma kwa bidii ambako kuliwezekana kutokana na kuaminiwa na familia na jamii kwa ujumla.

Licha ya mafanikio hayo bado hakuna usawa wa kipato na ajira jambo ambalo ni kikwazo cha ustawi wa mwanamke kwamba walisoma pamoja kwa kiwango sawa cha ufaulu, lakini kwenye ajira ndiyo kunakuwa na tofauti ya ujira na nafasi.

Bado kuna rushwa ya ngono ambayo ni kikwazo kikubwa kazini na vyuoni, wako waliokosa kazi kwa sababu hawakutoa rushwa hiyo, wako waliofelishwa kwa sababu hawakutoa rushwa hiyo, jambo hilo ni hatari sana kwa ustawi wa mwanamke.

Maadhimisho haya yawe chachu ya kuleta mabadiliko makubwa ya kifikra na ukombozi dhidi ya mwanamke ambaye naye ataikomboa jamii yake kipato chake kitaisaidia jamii.

Katika yote ni lazima watoto wa kiume wahusishwe, lazima vijana na wababa wahusishwe ili kutambua uhalisia nao kuwa sehemu ya suluhisho la kudumu, maana baadhi ya mambo yanatendwa nao bila kujua au ni kwa vile wamekuzwa hivyo.

***Tutafakari!***

# HARUSI







Harusi iliyofana kati ya Michael John na Loyce Joseph, ambayo ilifungwa siku ya Jumapili iliyopita katika kanisa la Sabato Kirumba jijini Mwanza. Sherehe ya aina yake ilifanyika katika ukumbi wa Gold Crest.





MITINDO







FURAHIA 'SIKU ZAKO'

# Mavazi haya yanakufanya ujiamini

WANAWAKE wengi wanakuwa na wasiwasi wakati anapoingia katika kipindi chao cha hedhi, mara nyingi huwa anapoteza umakini na hali ya kujiamini kama akikosa vazi la kujisitiri.

Upatikaji wa taulo za kike maarufu kama Sodo, imekuwa ya gharama kubwa na baadhi yao wanatumia njia za jadi kujitunza.

Wataalamu wa mavazi wanasema pamoja na kutumia njia zote mbili, aina ya nguo nazo ni jambo la muhimu kuliangalia ili kumuondolea hofu muhusika.

Inapendekezwa katika kipindi hiki kizito, ni vizuri mtu akachagua nguo za pamba zenye rangi nzito kama nyeusi, bluu iliyokoza au nyekundu.

Nguo hizi za rangi zina uwezo mkubwa wa kuhimili katika hali nzito, kwa kawaida huwa haionyeshi unyevunyevu kama zilizvyo za rangi nyingine.

Kama wewe ni mpenzi wa nguo za rangi nyeupe au zile za rangi hafifu , unashauriwa kuvaa koti refu au shati lisilopisha unyevu haraka.

Nguo zingine ambazo zinatoa uhuru zaini ni zile za Jeans ambazo zina rani nzito.

Kama unapitia ndani ya kipindi hicho, zingatia mambo hayo uliyoelezwa kwa ajili ya kuwa na furaha wakati wote.

URE MBO









## URE MBO WA KUCHA

# Si kujidai tu, huongeza kujiamini

UREMBO wa kucha ni jambo muhimu kwa kila mwanamke. Usafi wa kiungo hiki inakufanya uonekane mwenye utofauti na muonekano wa kupendeza.

Badhi ya wanawake katika kuremba zaidi, wanaamua kubandika kucha bandia ambazo wanaamini zitawapa matokeo bora kwa kuonekana mrembo.

Hata hivyo, wataalamu wa urembo wanashauri kwa wanawake wenye kucha zenye afya, njia ya kusafisha na kuzitunza kiasilia ni nzuri zaidi.



Wanasema njia ya kiasili inamfanya mtu kuwa na kucha zenye mng'aro, imara na zinazodumu kwa muda mrefu, kuliko zile za bandia.

Unaweza kutunza kucha zako na kuzifanya kuwa ngumu na zenye mvuto kwa kutumia mafuta ya mzaituni, maji na limao.

**JINSI YA KUANDAA**

Chukua mafuta ya mzaituni (Olive oil) kijiko kimoja, kijiko cha maji ya limao na maji ya vuguvugu.

Weka mchanganyiko huo katika chombo kisafi kisha koroga vizuri hadi uhakikishe imechanganyika.

Ukimaliza, chukua pamba halafu chovya kwenye mchannyiko wako na safisha kucha zako taratibu. Unashauriwa kusafisha usiku ili asubuhi usafishe kwa maji ya vuguvugu yaliyowekwa chumvi.

Fanya hivyo ndani ya wiki moja kwa ajili ya kupata matokeo ya haraka. Njia hii itapelekea kuwa na kucha nyeupe na zenye afya ambazo zitakufanya uwena na furaha muda wote.

Kwa ujumla urembo wa kucha humfanya mwanamke kujiamini zaidi na huongeza uhusiano na watu wengine katika maisha yake ya kila siku.

## MAPISHI

**Na Mary Geofrey**

# Pilipili ya kupikwa



PILIPILI ni kiungo kinachompa mlaji hamu ya kula chakula, kiungo hiki kinaweza kutumika katika chakula cha aina yoyote.



**MAANDALIZI**

Karoti tatu kubwa, Pilipili hoho moja, Vitunguu saumu vitatu, vitunguu maji vitano, tangawizi moja, majani ya giligiliani, ndimu na chumvi.

Mafuta kidogo sana, pilipili mbuzi tatu au utakavyopenda, nyanya tatu zilizoiva vizuri, pilipili ya unga vijiko viwili vikubwa vya chakula.

Oyster sauce kikombe kimoja cha kahawa, menya nyanya, hoho, karoti, vitunguu maji, vitunguu saumu, tangawizi, majani ya giligiliani yachambue.

**NAMNA YA KUANDAA**

Katakata vitunguu maji na nyanya weka bakuli tofauti, twanga vitunguu saumu na majani ya giligiliani, kwangua karoti pia katakata pilipili hoho.

Bandika mafuta jikoni yakipata moto weka vitunguu maji koroga dakika mbili weka vitunguu saumu na giligiliani koroga tia tangawizi kisha hoho na karoti.




Acha kidogo weka nyanya kisha weka pilipili ya unga na kisha kamulia ndimu, tia chumvi na funika mpaka nyanya iive vizuri. Baada ya kuweka pilipili weka oyster sauce acha ichemke kisha epua ili ipoe.

Ukiona imepoa iweke kwenye blenda isage hapo pilipili yako itakua tayari kwa ajili ya kuliwa.

MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya





# WASWAHILI husema, 'nyumbani ndipo moyo wa mtu ulipo'

Hii ina ukweli ndani yake kwa sababu nyumbani ndipo palipo na mkusanyiko wa maisha, kumbukumbu na upendo kwa asilimia kubwa ya watu.

Nasema hivyo kwa sababu, binadamu kila mmoja hujishughulisha na mambo mbalimbali lengo likiwa ni kujitafutia ridhiki na kuhakikisha mkono unakwenda kinywani na mambo mengine ya kifamilia yanakwenda sawa.

Lakini pamoja na kujishughulisha huko, lakini mwisho wa siku lazima arejee nyumbani kujipumzisha bila kujali umbali wake.

Hivyo basi, kwa vyovyote vile lazima uhakikishe nyumbani kunakuwa mahali sahihi, panapokuvutia kila siku na panafanyika kuwa nyumbani kwelikweli.

Na ili kuifanya nyumba iwe nyumbani zipo njia mbalimbali za kufanya ambazo hazihitaji gharama kubwa ya kifedha ambazo ni rahisi. Mojawapo ni mapambo ya ndani ya picha ambayo unaipenda na ukapamba.

Waswahili husema, 'picha inaongea', hivyo unaweza kutumia picha kuweka katika nyumba yako na badala ya kitu hicho kutegemea kukipata kwa binadamu, ukakipata kupitia picha hiyo.

Kwa mfano picha inayoonyesha alama ya upendo au yenye alama yoyote inayokukumbusha enzi ukiwa nyumbani kwenu ulikozaliwa. Picha hiyo siyo lazima uiweke ukutani, inaweza kuwekwa hata katika shelfu, juu ya meza, vitu kama hivyo vinaipa nyumba muonekano na hisia inayotambulisha familia.

Kitu kingine unachotakiwa kukiboresha kikufurahishe kujisikia uko nyumbani ni kwenye chumba cha kulala.

Chumba kinapowekwa vizuri, kisafi, kinachovutia na chenye utulivu wa aina yake, kinakuvutia pia kupapenda nyumbani.

Jambo jingine ni kuiweka nyumba yako katika upekee, kila nyumba ina upekee wake na mahitaji tofauti kuendana na wakaaji wake, hakikisha unapambana kuitafutia upekee.

Hakikisha nyumba yako inakuwa safi, hakuna vyombo vinavyoachwa vichafu iwe ni kwenye sinki, karo, beseni, ndoo na popote pale katika nyumba.

Nyumba safi inatakiwa iwe nadhifu nje na ndani na zipo kanuni zinazopaswa kuwekwa ili kuhakikisha hali hiyo ya usafi inaendelea.

Nenda na wakati kwa kuiweka nyumba katika hali ya wakati uliopo kuweka mapambo yanayoendana na wakati huo hususani katika vipindi vya sikukuu za mwisho wa mwaka.

Bila kusahau masuala ya mapishi, ili nyumbani au mtu ajisikie yuko nyumbani lazima kuwe kunapikwa chakula.

Nyumba isiyopikwa chakula au kukosa 'ubize' wa hapa na pale panachosha kukaa.

## MPANGILIO

### Dondoo namna ya kurembesha kitanda chumba cha kulala

**1:** Kiweke kitanda sehemu inayostahili, wengine wanapenda kuweka pembeni lakini baadhi wanapenda kuwa katikati katika ukuta wa mbele.


**2:** Tandika mashuka ya aina na rangi tofauti, mashuka laini hutandikwa chini na yale mazito huwekwa juu na sehemu ya miguu hushuka hadi chini.

**3:** Weka kapeti ndogo za kukanyagia miguu wakati wa kulala, wengine wanatumia ya vitambaa au ya manyoya.

**4:** Weka taa za kulalia pembeni ya kitanda chako, hii licha ya kupendezesha, pia itakusaidia kuwasha na kuzima kwa urahisi wakati wa usiku.



# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2020
SMS - 0621 412 879
JUKWAANI
MKE WANGU NILI-KUSHAURI TUPUMZIKE KUZAA TUWAACHIE VIJANA!
KWA JINSI WALIVYOKUWA BIZE, TUKIZUBAA DUNIA ITABAKI NA MITI TU!
MZEE ULITUMIA NGUVU KUBWA NA USHAWISHI MKUBWA NA ULISEMA IKITOKEA "UMEPIGWA CHALI" HUTOKUBALI
YALIKUWA MANENO YA KUNOGESHA MKUTANO 'USIBOE'
WAHUNI SIGARA MLIONILETEA MMEWEKA NINI MBONA NAJIKUTA NASHIRIKI RIADHA NA WATU WENGI?
JITAHIDI UWAPITE UWE WA KWANZA
TANDALE
BABY NINA NANIHII YAKO?
UNANINI? MIMBA AU UJAUZITO? WEEEEE.... AU HELA?
OKE NISHAURI NIISHI VIPI BAADA YA KUBWAGWA
KUNYWA MAJI MENGI, LALA SANA MCHANA NA USIPENDE KUSINZIA
NAKUHURUMUA UTAFUNGWA JELA UTAKUFA HUKO HUKO! ISITOSHE JELA SIO 'BUSTANI YA HEDEN' PUNGUZA WIVU!
ILA JANAMKE LAKO LILILONITIA HASARA KUNUNUA BUNDUKI NDIO 'BUSTANI YA HEDEN?' AU SIO!
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...MAISHA KIOO UKIYACHEKEA YANAKUCHEKEA...

HABARI KIMATAIFA

# Iran kulipiza kisasi cha mauaji ya mwanasayansi

**TEHRAN, Iran**

RAIS wa Iran, Hasan Rouhani, ameituhumu Israel kwa kuhusika na mauaji ya mwanasayansi wake wa nyuklia, lakini ameapa kutorudi nyuma katika mpango wa kurutubisha madini hayo.

Mwanasayansi huyo, Mohsen Fakhrizadeh, aliuawa nje ya mji mkuu wa Tehran, siku ya Ijumaa katika shambulio la kutupiana risasi.

Israel haijatoa tamko lolote kuhusiana na madai hayo, lakini iliwahi kumshtumu mwanasayansi huyo kwa kuhusika na mpango wa kisiri wa kuunda silaha za nyuklia.

Hata hivyo, kiongozi hiyo alisema makomando wa kijeshi wa Iran wameapa kulipiza kisasi mauaji hayo.

"Kwa mara nyigine tena, mikono ya maadui wa ulimwengu waliojawa na kiburi wametuulia mtu wetu," alisema Rais Hassan Rouhani kwa mujibu wa televisheni ya kitaifa.

"Mauaji ya shujaa Fakhrizadeh yanaonesha kuwa maadui wetu' walivyotetereka na kiwango chao cha chuki dhidi yetu,ushujaa wake hautarudisha nyuma mafanikio yetu." aliongeza

Fakhrizadeh alifariki baada ya kufikishwa hospitali kutokana na majeraha hayo yaliyosababishwa na shambulizi hilo lililotokea eneo la Absard, Mkoa wa Damavand.

Hossein Dehghan, mshauri wa kijeshi wa kiongozi mkuu wa kidini wa Iran, Ayatollah Ali Khamenei, aliapa kuwashambulia walitekeleza mauaji hayo.

Iran inasisitiza mpango wake wa nyuklia ni salama na lengo lake ni la amani.

Waziri wa Mambo ya Nje wa nchi hiyo, Mohammad Javad Zarif, amelaani mauaji hayo na kuelezea ni kitendo cha ugaidi.

Mashirika ya ujasusi kutoka nchi za Magharibi, yanaamini Fakhrizadeh, alikuwa mtu anayesimamia mpango wa kisiri wa uundaji silaha za nyuklia.

Taarifa ya mauaji hayo zinakuja wakati kumekuwa na hofu mpya kuhusu uzalishaji wa madini ya urani unaofanywa na nchi hiyo.

Madini ya urani ni kiungo muhimu katika utengenezaji wa nishati ya nyuklia na silaha za kijeshi za kinyuklia.

Mkataba wa mwaka 2015 uliofikiwa na nchi sita zenye uwezo duniani, uliweka kiwango cha ukuzaji wa madini hayo, lakini Rais wa Marekani, Donald Trump alijiondoa mwaka 2018, na kusababisha ukiukaji wa makubaliano hayo.

Hata hivyo, Rais mteule Joe Biden, alikubali kushauriana na Iran atakapoingia rasmi madarakani mwezi Januari mwakani.

Kati ya mwaka 2010 na 2012, wanasayansi wanne wa nyuklia wa nchi hiyo wameuawa, huku Iran ikiilaumu Israel kwa kuhusika na mauaji hayo.

Jina la Fakhrizadeh lilitajwa na Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, katika maelezo yake kuhusu mpango wa nyuklia wa nchi hiyo aliyoitoa mwezi April mwaka jana.

Katika taarifa iliyotolewa juzi, Wizara ya Ulinzi ya Iran ilisema magaidi waliojihami walilenga gari lililokuwa limembeba Mohsen Fakhrizadeh, ambaye ni mkuu wa wizara hiyo katika shirika la utafiti na uvumbuzi.

"Baada ya makabiliano ya risasi kati ya magaidi hao na walinzi wake, Fakhrizadeh alijeruhiwa vibaya na alikimbizwa hospitali."Kwa bahati mbaya jitihada za madaktari kuokoa maisha yake hazikufanikiwa na muda mfupi baadaye akafariki." Alisema Waziri huyo.

Taarifa za vyombo vya habari nchini Iran zinasema washambuliaji walipiga risasi mfululizo gari la mwanasayansi huyo.

**BBC**



Mwanasayansi wa Iran, Mohsen Fakhrizadeh, wakati wa uhai wake katika picha ndogo, chini ni gari ambalo lilishambuliwa na kusababisha kifo chake. **(PICHA: AFP)**

# Viongozi SADC waijadili Msumbiji

**GABORONE, Botswana**

WAKUU wa nchi zilizo kusini mwa Afrika, wamekutana katika mkutano wa dharura kujadili suala la usalama wa ukanda huo.

Viongozi hao wamekubaliana kushirikiana katika kupambana na uasi wa wanamgambo wenye itikadi kali za kidini uliozuka katika sehemu ya kaskazini mwa Msumbiji.

Hata hivyo, hawakutoa maelezo zaidi juu ya hatua wanazopanga kuchukua kukabiliana na kitisho hicho cha ugaidi.

Katika taarifa ya viongozi hao walisema wana wasiwasi kuhusu matukio ya kigaidi nchini humo hasa katika jimbo la Cabo Delgado.

Wanamgambo wa Kiislamu wenye itikadi kali wamekuwa wakifanya mashambulizi kwa miaka mitatu katika jimbo hilo.

Lakini katika miezi ya hivi karibu mashambulizi hayo yaliongezeka na kuzindua utawala wa kikhalifa katika jimbo hilo la Capo Delgado.

**DW**

## Rais azuiwa na begi lililojaa fedha

**TEGUCIGALPA, Honduras**

RAIS wa zamani wa Honduras, Manuel Zelaya, amesema alizuiwa katika uwanja wa ndege wa Tegucigalpa, akiwa na dola 18,000 kwenye begi lake.

Zelaya alisema aliachiwa huru masaa matatu baadaye, kulingana na gazeti la nchini humo La Tribuna.

Katika ukurasa wake wa Twitter, kiongozi huyo alidai kuwa pesa hizo sio zake, na alikuwa amepanga kwenda nchini Mexico kwenye semina.

Sheria za nchi hiyo inamzuia msafiri yoyote kutobeba fedha zaidi ya dola 10,000.

Akiwa amezuiwa katika uwanja huo wa ndege, nje kulizuka maandamano ya wananchi ambao walitanywa na polisi kwa kuwarushia mabomu ya machozi.

Zelaya alikuwa akfanya biashara ya mbao kabla ya kuwa mkuu wa nchi hiyo mwaka 2006.

Aliondolewa madarakani mwaka 2009, lakini kwa sasa ni kiongozi wa chama cha upinzani.

**DW**

## Watu sita wauawa Iraq

**BAGHDAD, Iraq**

WATU sita wameuawa katika mapigano yaliyoibuka kati ya makundi ya waandamanaji wanaopingana nchini Iraq.

Maofisa wa usalama walisema jana kuwa tukio hilo limetokea katika mji wa Nasiriyah ulio kusini mwa nchi hiyo, kati ya makundi mawili yanayopingana.

Makundi hayo ni lile la wanachama wa vuguvugu la Oktoba 2019 linaloendesha maandamano ya kuipinga serikali, na la wafuasi wa kiongozi wa kidini wa madhehebu ya Kishia nchini humo, Moqtada Sadr.

Katika mji huo, wanaharakati wa vuguvugu hilo la kuipinga serikali waliwashtumu wafuasi wa Sadr kwa kuwafyatulia risasi na kuchoma moto mahema yao.

**DW**

MAKALA

# Kujitolea kunalipa



Na Magabilo Masambu

MIAKA ya nyuma kidogo katika taifa letu, kujitolea lilikuwa jambo la kawaida ikilinganishwa na sasa. Inaonekana vijana wengi wa leo si rahisi sana kufanya kazi zisizo za malipo.Wapo wanaolaumu kwamba pengine inawezekana ni malezi mabovu.Wengine husema maisha yamebadilika na kuwa magumu zaidi, kwahiyo fedha imekuwa kila kitu ikilinganishwa na hapo zamani ambapo, vitu vingi kama mazao na chakula kwa ujumla vilipatikana kwa urahisi.Hoja zao zote ni za msingi lakini hatuwezi kabisa kuacha kujitolea katika jamii zetu kwasababu kujitolea kuna faida nyingi.

Moja hujenga mahusiano yasio na kikomo. Mahusiano yanayojengwa kwa misingi ya malipo huwa yanaishia pale malipo yanapofanyika. Baada ya hapo, mahusiano huwa hayapo tena.

Lakini kujitolea hasa katika jamii kunatengeneza mazingira ya kuwa na mahusiano mazuri na jamii inayokuzunguka, kiasi kwamba mahusiano hayo hayatakuwa yenye mipaka kwasababu jamii inakuwa na deni kwako la kulipa wema unaofanya katika jamii hiyo, ambapo ni vigumu sana kuweza kulipa wema wa mtu usio wenye makubaliano ya kifedha.

Pili, kusaidia kutatua matatizo ya jamii. Maisha ni zaidi ya fedha. Mtazamo huu unaweza kuzua mjadala mkubwa kutokana na tofauti za kifikra kuhusu uhusiano wa fedha na maisha.

Lakini upo ukweli kwamba fedha si kila kitu pamoja na kwamba fedha ni muhimu. Hatuishi kwa lengo la kujikusanyia fedha, kujiletea faida binafsi pekee ingawa ni kweli tunahitaji fedha ili kufanya mahitaji. Kujitolea, kwa mantiki hii ni kuelewa kuwa si lazima ubadilishane ujuzi na muda wako kwa vipande vya fedha. Wakati mwingine waweza kutoa ujuzi, maarifa na nguvu zako kwa lengo tu la kutafuta furaha ya kutoa mchango wako katika kuboresha maisha ya wengine, ambao katika hali ya kawaida wasingeweza kunufaika na ujuzi huo bila kukulipa.

Tatu, kujenga uaminifu. Unapofanya kazi za kujitolea jamii inaamini kuwa ukipata kazi ya malipo utaifanya vizuri, hivyo unaweka mazingira ya jamii na waajiri kukuamini zaidi kiasi kwamba itakufanya uweze kupata kazi za malipo mapema kuliko kama ungesubiri upate kazi za kulipwa.

Pia inakujengea mazingira ya kufanya kazi hata malipo yakiwa kidogo, utakuwa tayari kufanya kazi tu kwakuwa kama uliweza kufanya kazi za kujitolea huwezi kushindwa kufanya kazi zenye malipo kidogo.

Kujifunza ujuzi bila gharama. Si kila ujuzi unaohitajika kazini unapatikana vyuoni.

Mara nyingi vyuo hutufunza maarifa ya jumla yanayoweza yasionekane kabisa na matakwa ya soko la ajira.

Hii ni kwa sababu si rahisi vyuo kufanya utafiti wa mara kwa mara kubaini mahitaji ya soko la ajira kwa minajili ya kurekebisha mitaala yao. Kadhalika, ni vigumu kwa mfumo wa elimu kukidhi mahitaji mahususi ya kila mhitimu na kila mwajiri. Kwa sababu hiyo, vyuo hujikuta vikifundisha maarifa ya jumla ambayo katika hali halisi yanaweza yasikidhi mahitaji ya waajiri.

Kujitolea hutusaidia kujifunza ujuzi mahusus unaohitajika ili kuajirika kirahisi bila kulazimika kuulipia kwa fedha, isipokuwa kwa kutumia nguvu na muda wetu. Kwa mfano, mhitimu wa teknolojia ya mawasiliano anaweza kujitolea kufanya kazi katika kampuni ya mawasiliano na hivyo kujifunza mambo mengi ambayo huenda hakujifunza akiwa chuoni.

Kwa kutoa muda na nguvu zake bila kutarajia malipo, mhitimu huyu hupata faida ya kujiongezea nafasi ya kuajirika pale nafasi za kazi zinapojitokeza.

Kujitafutia uzoefu unaohitajika. Waajiri wengi huweka sharti la waombaji kuonesha uzoefu wa kazi wanayoiomba, kama ushahidi wa uwezo wa kumudu kazi husika. Jambo hili kwa hakika ni kikwazo kwa waombaji wengi hasa wanaotoka vyuoni moja kwa moja, kwasababu ni kweli huwa hawajawahi kuajiriwa na hivyo hawana uzoefu. Pamoja na ugumu wa sharti hili la uzoefu, bado litaendelea kuwa sehemu muhimu ya matangazo ya ajira.

Kujitolea kunaweza kuwa sehemu ya suluhisho la sharti hili. Unapojitolea bila malipo, unajitengenezea uzoefu utakaohitajika na mwajiri bila kulazimika kuajiriwa. Kujenga tabia ya kujitolea ni kuchukua hatua za makusudi kupambana na sharti hili.

Kwa kutokutambua umuhimu wa kujitolea, wahitimu wengi wamekuwa wakitumia muda mwingi kulalamikia sharti la uzoefu wakati katika hali halisi hawafanyi chochote kukabiliana na changamoto hiyo.

**Itaendelea juma lijalo.......**

**0689157789**
**Magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# DJ Emperor 'Kusaga', Sly, walivyorusha watu 'majoka'



Na Adam Fungamwango

WIKI iliyopita tulikuwa na mada iliyoonyesha jiji la Dar es Salaam lilivyokuwa linachemka kama bahari, huku kumbi za starehe zikiwa kwenye pilikapilika kila wikiendi. Tuliziangalia zaidi kumbi za dansi ambazo bendi mbalimbali zilikuwa zikijivinjari.

Leo tunatoka kidogo kwenye dansi, tunaangalia madisco. Leo tutapiga ndege wawili kwa jiwe moja. Tutawaangalia ma-DJ waliokuwa wakitamba wakati huo pamoja na kumbi za starehe ambazo zilikuwa zinapigwa ngoma hizo.

Disko ni mchanganyiko wa muziki mbalimbali kutoka pande zote za dunia. Ni muziki kutoka mabara yote ya dunia hii. Tofauti na muziki wa dansi ambao ulikuwa bendi tu ambazo zilikuwa zinapiga 'live'. DisKo ni muziki ambao ulitoka kwenye santuri zilizokuwa zimerekodiwa.

Wasimamizi wa mashine na watia mbwembwe ambao walikuwa wakizipiga nyimbo hizo ndiyo wanaitwa ma-DJ.

Ilikuwa miaka ya 1970 hadi mwanzoni mwa miaka ya 1990 disko lilivuma kama moto wa nyika, wenyewe watoto wa mjini waliita 'kuruka majoka', au 'kuruka ndebe.'

Halafu kulikuwa na disco la wanafunzi wa shule za msingi na sekondari ambalo lilikuwa likipigwa mchana mpaka jioni, na hata kama ikifika usiku, unakuwa ni wa kawaida tu saa mbili mwisho.

Disco hili liliitwa 'boogie'. Ikumbukwe kuwa ilikuwa si rahisi wakati huo wazazi kuwaruhusu vijana wao kwenda disco hata mchana, achilia mbali usiku, ndiyo maana kulikuwa na madisco ya mchana kwa wanafunzi.

Kwa kuwa hakukuwa na ruhusa, ilibidi kila mwanafunzi apambane na hali yake kujua atatokaje, au kutorokaje kwenda disco. Baadhi ya wazazi walidanganywa na kutoa ruhusa kwa watoto wao, lakini wengi hawakuwa na ruhusa.

Aliyekwenda disco, kama mwanafunzi ilibidi kwanza awe na kiingilio na nauli ya UDA kwenda na kurudi nyumbani.

Kwa wakati ule zilipatikana kwa kubania pesa ambazo mwanafunzi anapewa za kujikimu shuleni, pamoja na baadhi ya wageni wanaokuja nyumbani. Kama haitoshi basi ni lazima utembee kwa miguu wakati wa kwenda, ila kurudi kwa sababu giza limeingia ni lazima mtu arudi kwa basi.

Na madisko mengi ya wanafunzi yalikuwa yakianzia saa tisa mchana. Katikati ya Jiji kulikucha. Kulikuwa na ma-DJ ambao baadhi yao walikuwa wamefika Ulaya au 'mamtoni' walivyokuwa wakiita, ambapo wakati huo ilikuwa ni ngumu sana kukutana na watu waliofika huko.

Wachache wao ni mabaharia ambao nao kwa kulitambua hiyo, walikuwa na mbwembwe za aina yake, huku wakiwa na nguo au 'viwalo' tofauti na watu wengine.

Tuaanza na mtu mmoja anaitwa DJ Emperor. Huyu alitesa sana na kuwarukisha watu majoka kwenye maeneo ya New Afrika Hotel ghorofa ya saba. DJ Emperor ndiyo huyu Joseph Kusaga mmiliki wa Clouds. Kulikuwa pia na DJ Bonny Love.

Ukienda Motel Agip unakutana na DJ Luke pamoja na DJ Composer ambao nao walikuwa wakitesa kwenye eneo lao.

Kwenye kumbi ya YMCA kulikuwa na DJ Choggy Sly na DJ Kalikali. Ukumbi wa Mbowe Hotels kulikuwa na disco linaloitwa Space 1900 Discotheque na ma-DJ kibao walikuwa pale kama DJ Chriss Phabby the Lover, DJ, Super Deo Mcghee na DJ Joe Johnson Holela.

Baadaye waliondoka Mbowe na kuhamia YMCA na pale ikaanzishwa RSVR, chini ya ma-DJ wengine kabisa ambao nao walivuma kweli kweli kama DJ Seydou na DJ Jerry Kotto.

Hawa walikuwa watoto wa mjini kweli kweli na walikuwa mara nyingi ni wa kwanza kupata ngoma mpya za mamtoni, ukumbi wa Mbowe ukawa ndiyo unaopendwa mno na vijana wa mjini.

DJ Emperor 'Kusaga' akaja tena kutamba kwenye kumbi za Mawingu, Sew View na TAZARA Club akiwa na DJ Mao, na maeneo ya katikati ya jiji kwa watoto wa 'kidosi' maeneo ya Upanga, Oysterbay, Pink Coconut, Salender Bridge kulikuwa na DJ Ajib, DJ Luke na Jesse Mwalongo.

Maeneo ya Kariakoo mtaa wa Uhuru, Keys Hotel kulikuwa na disco kabambe chini ya DJ Eddy Sally na DJ Sweet Francis, Kilimanjaro Pool Side nayo ikawa na DJ Flesh na DJ Mshua.

Kuna ukumbi mmoja maarufu tangu enzi wa ukoloni unaitwa Maggot, baadaye Washirika, kulikuwa na disco la DJ Bubu. Yeye aliitwa hivyo kwa sababu ni ngoma tu mwanzo mwisho, hakuna kuongea.

Jet Set Discotheque kulikuwa na DJ Rusual na DJ Young Omar, Moon Dust Discotheque, Mwananyamala na baadae Lan'gata, Kinondoni alikuwepo DJ Young Kim (Kim & the Boyz). DJ Kim.

Villa Hotel, Mwananyamala alikuwapo DJ Young Millionaire na Captain Ngomeley.

Miaka ya katikati ya 1980 madisko yakaanza kusambaa kwenye hoteli za ufukweni.

Rungwe Oceanic Hotels ya Mzee Mwakitwange kulikuwa na DJ Ngomeley na DJ Roma Pop Juice,

Silversands kulikuwa na DJ John Peter Pantalakis, Club Africana, na DJ Mehboob na DJ John Bure.

Msasani Beach Club, iliyokuwa maarufu sana, alikuwepo mtoto wa mjini DJ Nasser na DJ Nigga J, ndiyo huyu mtangazaji Masoud Masoud.

# HADITHI

WASWAHILI wanasema mshika mawili moja humponyoka na karamu mbili zilimshinda fisi. Cecilia, msichana mwenye kila sifa ya kuitwa msichana mrembo, anaangukia kwenye mapenzi ya vijana wawili. Mmoja ni fukara na mwingine mwenye uwezo. Kutokana na mwenyewe Cecilia kutokuwa na msimamo wenye kueleweka, anawaingiza vijana hao kwenye chuki na visasi, vilivyoambatana na wivu uliopindukia na kusababisha maafa makubwa. Ni kisa cha kusikitisha, kutisha na kuhuzunisha, lakini chenye elimu kubwa.

# Adui Namba Moja-10

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

JINSI walivyoongozana, wakiwa na tabasamu na bashasha, hata kipofu angejua kuwa ni wapenzi.

"Huyu ndiye Mashaka. Leo atanitambua." Alijisemea akiwa na hasira zilizokaribia kuupasua mwili na moyo wake.

Alijipapasa mfukoni, bastola yake ilikuwapo. Akili ilikuwa imemruka. Alikuwa akitamani sehemu ambayo yule kijana yupo, awepo yeye. Alikuwa kama akiota ndoto mbaya.

"Cecy, kumbe hicho ndicho kibwana chako kinachokuzuzua, sasa ngoja nikiondoe, tuone utakwenda kwa nani. Ni lazima utarudi kwangu tu. Hutokuwa na janja tena." Alisema kwa sauti ndani ya gari, lakini alikuwa peke yake. Alijiambia mwenyewe.

Mapozi ya wapenzi hao walizidi kumtia uchizi Zahir, foleni ilianza kutembea. Alichofanya kuliweka gari pembeni, akateremka. Akatembea taratibu huku macho yake yakiwa mbele ili asipoteze mawindo yake.

Mashaka na Cecy, tayari alikuwa wamefika kituoni. Ilikuwa ni majira ya saa 12:00 jioni. Kulikuwa na umati mkubwa wa watu kituoni hapo. Kila mmoja alikuwa na mambo yake. Hakuna aliyekuwa akimfuatilia mwenzake anafanya nini.

Mashaka na Cecy tayari walikuwa wamesimama kituoni, lengo ni kupanda basi kwenda Ilala Mchikichini kufuata mahitaji ambayo waliyataka.

Walikuwa wakilishana tambi walizonunua pembeni kwa barabara. Hakuna aliyemuona Zahir ambaye aliwapita ghafla na baadaye kuvuka barabara. Akasimama katikati ya barabara mbili za Kawawa. Akatoa bastola na kumlenga Mashaka. Akaachia risasi moja tu, iliyomrusha hatua kadhaa nyuma na kuzua taftarani kituoni hapo.

***************************

Wiki moja baada ya mazishi ya Mashaka, Cecy alikuwa bado hajielewi. Bado alidhani kuwa ilikuwa ndoto mbaya ambayo anaendelea kuiota. Akili yake ilikataa kwamba ni kweli mpenzi wake Mashaka alikuwa ameuawa.

"Ameuawa na nani?" Hilo ndilo swali lililokuwa linamtatiza. Alifahamu kabisa kuwa Mashaka ni kijana ambaye hakuna mkorofi. Hakuna na matatizo na mtu yoyote. Sasa hadi kufikia mtu kuamua kulipa kisasi ni nini kimetokea? Akili yake ilihamia kwa Zahir.




**"Zahir anaweza kufanya hivi?" Alijiuliza. Ni kweli Zahir ni kijana mkorofi, mjivuni, lakini hakudhani kama anaweza kuwa katili kiasi hiki. 'Siamini kama ni yeye?" Hata hivyo aliamua kufanya uchunguzi. Ghafla simu iliita. Namba ilikuwa ni ya Zahir. "Bibie bado unaomboleza msiba wa bwana 'ako?" Ilikuwa bado kidogo amsemee ovyo.**

"Zahir anaweza kufanya hivi?" Alijiuliza. Ni kweli Zahir ni kijana mkorofi, mjivuni, lakini hakudhani kama anaweza kuwa katili kiasi hiki. 'Siamini kama ni yeye?" Hata hivyo aliamua kufanya uchunguzi. Ghafla simu iliita. Namba ilikuwa ni ya Zahir.

"Bibie bado unaomboleza msiba wa bwana 'ako?" Ilikuwa bado kidogo amsemee ovyo.

"Huyu vipi? Yaani kijana wa watu amefariki dunia badala ya kuonyesha kuhuzunika, lakini yeye anaongea maneno haya bila chembe ya huzuni kama aliyekufa ni mbwa?" Alijiuliza mwenyewe.

Cecy alizuia hasira zake akajibu "Hapana, nipo tu, kichwa kinanuma sana." "Njoo Coconut Hotel leo saa 12:00 jioni uondoe mawazo, bwana'ako ameshakufa, huna mwingine tena zaidi ya mimi."

Maneno yale bado yalizidi kumtia wazimu Cecy. Aliona kama vile Zahir alionyesha kufurahiwa na kifo cha Mashaka. Ilionekana kama vile kijana yule alikuwa kikwazo kwake.

Ni maneno ambayo yalimfanya Cecy awe makini zaidi na akajikuta akisema "Haya nakuja."

Hotel hiyo ilikuwa maeneo ya Keko Furniture jijini Dar es Salaam. Majira ya saa 12:45, Cecy aliingia, akiwa amejipamba akapambika mtoto wa watu. Nywele kama mzungu, huku akiwa amejipulizia mafuta mazuri ya kunukia kutoka Uarabuni. Kila aliyepishana naye, aligeuka na kumtazama, akisifia uumbaji wa Mwenyezi Mungu.

"Karibu." Ilikuwa ni sauti ya Zahir alimkaribisha.

"Ahsante." Alijibu akijilazimisha tabasamu, lakini akili yake haikuwa hapo. Iliwaza mengi.

Cecy, alimdanganya Zahir kuwa anaumwa kichwa, hivyo asingeweza kunywa pombe.

Kwa upande wa Zahir wala haikuwa tatizo kubwa kwake. Alichokuwa akitaka Cecy awepo tu pale, anywe asinywe hilo si tatizo.

Kwa furaha ya kumpata tena Cecy, alifakamia pombe kama maji.

"Mambo si hayo, bila kumfanya vile yule boya, nisingekupata." Zahir alianza kuropoka.

"Kwani umemfanyaje?" Aliuliza Cecy taratibu, hakutaka kushtuka ili kutomuogopesha Zahir.

"Hapa si mahali pazuri, kuna chumba nimechukua, twende tukaongee, askari wanaweza kusikia."

"Askari wanaweza kusikia." Ni maneno yaliyojaa kwenye kichwa cha Cecy. Yalikuwa yakijirudiarudia na kuzidi kumpa hasira. Alianza kutambua kuwa huenda kifo cha Mashaka kilikuwa na mkono wa Zahir. Na hilo ndilo alikuwa akilihitaji.

Alimnyanyua na kumkokota kwenda kwenye chumba namba 25 ambacho kilikodiwa. Zahir alionekana amezidiwa mno na kinywaji.

"Niambie, niambie, kifo cha Mashaka ni wewe unahusika au?"

"Yule boya tu, nimemuua mimi mwenyewe. Sijatuma mtu. Nimemuua mimi mwenyewe kwa mkono wangu na bastola hii hapa..." Aliongea kwa sauti ya kilevi, lakini ikionekana kabisa ana uhakika na anachokisema.

Zahir alimhadithia hatua moja mpaka nyingine aliyotumia hadi kumwondoa duniani Mashaka.

Jasho lilimtoka Cecy, nusura azimie. Alijiona ni kama yeye ndiye aliyemuua Mashaka. Hasira zilizidi kumpanda. Ni kama alipandisha mashetani hivi. Alimsukuma Zahir kwa nguvu akaangukia kitandani.

Hakuwa na nguvu yoyote kutokana na kuzidiwa zaidi na pombe. Kila dakika zilivyozidi kusonga mbele ndiyo ilionekana analewa zaidi kiasi cha kutaka kutokwa na fahamu.

Cecy akauendea mkoba wake. Akaufungua. Akachukua kitu ambacho alitaka kuchukua. Akaufunga mkoba. Akamuangalia Zahir kwa namna polisi anavyomwangalia jambazi. Zahir hakung'amua hilo.

Aliondoa baadhi ya nguo zake na kumwendea kimahaba. Kutokana na ulevi, Zahir hakuona kitu ambacho alishika Cecy mkononi.

Badala yake alimuona mwanamke huyo alimwangukia kitandani na kuhisi kugusana na ngozi nyororo, ilianza kumpapasa na kumfariji.

Na kweli alifarijika. Ghafla alihisi kitu kama sindano hivi ikimchoma kwenye mbavu. Awali maumivu hayakuwa makubwa sana. Baadaye alihisi maumivi makali ambayo hayavumiliki. Aliamua kuona nguvu zimwisha. Hakujua nini kimetokea. Alitaka kupiga kelele. Lakini mkono na Cecy ulitua kwenye mdomo wake na kuuziba.

Pombe na maumivu makali yalisababisha nguvu zizidi kupungua na kutoweza kabisa kuutoa mkono wake.

Alihisi kitu kingine kikipenya kwenye kifuani na kumfanya ajihisi kama anapaa. Halafu anaanguka kwenye shimo lisilokuwa na kina.

"Mpumbavu mkubwa wee. Yaani umuue mpenzi wangu mimi nikuache. Mashaka mpenzi wangu nimelipa. Nimekulipia. Niliacha siku nakuzika kuwa yoyote atakayekuwa amekuua sitomuacha salama." Alisema huku akikusanya alichotaka kukusanya.

**INAENDELEA JUMAPILI**



# AUNTY AJIFUNGUA MTOTO WA PILI

MSANII mkongwe wa filamu nchini, Aunty Ezekiel, amejifungua salama mtoto wa kiume.

Huyo ni mtoto wake wa pili, japo bado haijafahamika rasmi ni nani baba halali wa mtoto huyo, mtoto wake wa kwanza wa kike anafahamika kwa jina la Cookie, baba yake ni Mose Iyobo.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram ameweka taarifa hiyo kwa kuandika kuwa "Asante mungu kwa hii zawadi".

Baada ya kuweka posti hiyo, baadhi ya wasanii wakubwa walimiminika kumpatia pongezi.

Wema Sepetu aliandika ""Unajishaua jamani uwiii, hongera baby", huku Elizabeth Michael alimpongeza kwa kusema "Hongera my love".

Billnass akamwagia sifa na kumtahadharisha "Hongera sana boss wangu, ila chonde chonde kama ni wa kiume usije ukarogwa ukampa jina la Idris" na Monalisa amesema "Hongera sana mama wawili, jitahidi unifikie basi"

## Choki kwa watoto hawa, hongera!

MWANAMUZIKI wa dansi nchini, Ali Choki, amesema watoto wake wapo 9 kwa mama tofauti.

Akizungumza na EATV, Choki amesema kati ya watoto hao amepata wajukuu watatu, ambao anaendelea kuwalea.

"Kusema ukweli mimi nina watoto wengi jumla yake wapo 9 na wajukuu watatu, kwenye kutafufuta unaweza kuwa na mama tofauti lakini cha umuhimu watoto wako unawajua, kwa kipindi cha ujana nilikuwa naishi sehemu nyingi lakini sasa hivi tumeshakuwa watu wazima, unaamua kutulia na kulea watoto wako" amesema Ali Choki




## Nikki wa Pili hakwepeshagi ukweli

MWANAMUZIKI mkali wa HipHop, Nikki wa Pili, amemwagia sifa rapa mwenzake Young Lunya, kuwa amevuka mipaka kwa kutumia 'digital platform' kwa wasanii wanaochipukia.

"Msanii mchanga wa HipHop anapokuwa anaanza inabidi awe na mipaka ya kuvuka mbele, mfano Whozu alitumia 'digital platform' kutoka, mpaka sasa Young Lunya ndiyo ameweza kuvuka mipaka kwa kutumia 'digital', ameenda mbele ya kuwaza kurap ili wengine wafikirie zaidi biashara ili waweze kupenya"

Aidha Nikki wa Pili ameongeza kusema "Rap sio rahisi kuishika, wasanii wengi wa rap hawana uwezo au hawana watu wa kuwasogeza, mfano Young Lunya ametumia ujanja hata nyimbo zake zimebebwa kutokana na ubunifu wake,"



# Klopp ataka Wijnaldum kubaki Liver

**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp ana matumaini, Georginio Wijnaldum ataongeza mkataba wake wa kubaki Liverpool.


Wijnaldum mkataba wake wa sasa na mabingwa hao wa Ligi Kuu ya England unamalizika mwishoni mwa msimu huu na kiungo huyo amekuwa akihusishwa na Barcelona.

Kabla ya mchezo wake wa jana Jumamosi wa Ligi Kuu ya England dhidi ya Brighton and Hove Albion, Klopp alisema hakuna chochote anachojua kuhusu nyota huyo wa kimataifa wa Uholanzi, lakini angependa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 kubakia pale kwenye dimba la Anfield.

"Kiukweli siwezi kusema mengi kuhusu hilo. Nitakuwa na furaha kama atabakia hapa na hilo ndio jambo pekee," alisema.

"Lakini kukaa hapa, nina furaha kubwa na Gini, ningependa kuendelea kumuona kwenye kikosi changu katika kila mechi."

Wijnaldum aliwasili pale Liverpool akitokea Newcastle United mwaka 2016 na ameisaidia timu hiyo kushinda taji la Ligi Kuu, Ligi ya mabingwa Ulaya, UEFA Super na klabu bingwa ya Dunia.




# FLICK ATAKA KIWANGO KWA SANE



**MUNICH,** Ujerumani

KOCHA wa Bayern Munich, Hansi Flick, anataka kuona kiwango zaidi kutoka kwa Leroy Sane, lakini amesema straika huyo anahitaji muda.

Tangu alipojiunga na Bayern kutoka Manchester City kwa ada iliyoripotiwa kuwa ni euro milioni 45 mapema mwaka huu, Sane amefunga mabao matano na kutoa pasi za mwisho mbili kwenye mechi tisa.

Sane alikosa karibia msimu mzima wa 2019-20 akiwa na City baada ya kuumia goti. Wakati Flick akiwa anataka Sane kuimarika zaidi, lakini pia amejiandaa kuwa mvumilivu kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 kutokana na majeruhi.

"Yupo fiti kwa asilimia 100. Uwezo wake ni mkubwa," alisema Flick akiwaambia waandishi wa habari."Lakini kama ilivyo kwa wachezaji wengine, alipoteza mipira mingi kizembe katika mchezo dhidi ya Salzburg na anaonekana kuwa bado anahitaji muda. "Kuna sababu ya hilo na nimezungumza nae kuhusu hilo. Atajaribu kuwa bora wakati ujao."

# *Al Ahly yatwaa ubingwa wa 9 Afrika*

**CAIRO,** Misri

BAO la dakika za majeruhi kutoka kwa Mohamed Magdy liliipa Al Ahly ushindi dhidi ya wapinzani wao wa jiji moja la Cairo, Zamalek katika fainali ya kwanza ya mchezo mmoja kwenye Ligi ya mabingwa Afrika.

Mchezo huo ambao umetajwa kama 'fainali ya karne' kati ya miamba hao wa Cairo, ulionekana kama ungekwenda katika muda wa ziada.

Lakini Magdy alifunga bao hilo dakika ya 88 kwenye mchezo huo uliokuwa wa kuvutia, baada ya timu yake kuanza kuongoza kwa bao la Amr El Sulaya, kabla ya Shikabala kusawazisha.

Ahly wangeweza kuongoza tena wakati shuti la Elshahat lilipogonga mwamba akiwa amebakia yeye na kipa tu.

Ushindi huo umeendeleza rekodi na sasa wamekuwa mabingwa wa Ligi ya mabingwa Afrika kwa mara ya tisa.

Na pia kocha wao Pitso Mosimane raia wa Afrika Kusini, amekuwa kocha wa tatu kushinda taji hilo na klabu mbili tofauti.



HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# NI LAMPARD VS MOURINHO LEO

### ●●● Mourinho aliinoa Chelsea katika vipindi viwili tofauti, alimfundisha Lampard, amesema...

**LONDON,** England

KOCHA Mkuu wa Tottenham Hotspur, Jose Mourinho, amebainisha kwamba, Frank Lampard alikuwa kwenye presha kubwa baada ya Chelsea kutumia fedha nyingi katika usajili msimu huu.

**Mourinho na Spurs yake wapo kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu wakati leo Jumapili wakishuka dimbani kucheza na wapinzani wao wa jiji moja la London, Chelsea pale kwenye dimba la Stamford Bridge.**

Baada ya kuwasajili wachezaji kama Kai Havertz, Timo Werner, Ben Chilwell, Hakim Ziyech na Edouard Mendy, Chelsea wapo nafasi ya tatu kwenye msimamo.

Usajili huyo umeripotiwa kuwagharimu Chelsea pauni milioni 222 ukiwa ni uwezekaji mkubwa zaidi kwa kikosi hicho cha Lampard ambaye yupo kwenye msimu wake wa pili.

Mourinho, ambaye aliinoa Chelsea katika vipindi viwili tofauti na alimfundisha Lampard, amesema usajili huo ulimpa presha.

"Wakati unapopewa nafsi kubwa ya kushinda, unajua kwanini unapewa nafasi hiyo," alisema Mourinho akiwaambia waandishi wa habari.

"Na unatakiwa kukubali hilo na unatakiwa kudili na hali hiyo ya presha kadili unavyoweza.

"Nilikuwa kwenye klabu ambazo zilikuwa hivyo, tuseme bingwa wa sokoni kwa sababu ya uwezekaji mkubwa.

"Nililazimika kudili na presha ile kubwa. "Hivyo, ni jambo la kawaida kwa kocha kuwa na presha wakati timu inapofanya uwezekaji mkubwa wa kusajili wachezaji."

Spurs pia iliimarisha kikosi chake mwaka jana, ingawa usajili mwingine ulifanywa kabla ya Mourinho kuchukua mikoba ya Mauricio Pochettino miezi 12 iliyopita.

Wachezaji kama Tanguy Ndombele, Giovani Lo Celso, Steven Bergwijn, Ryan Sessegnon, Sergio Reguilon, Pierre-Emile Hojbjerg na Matt Doherty wamewasili pale Tottenham stangu mwaka 2019.

## ZISIKUPITE

### HAALAND HAONDOKI

MKURUGENZI wa michezo wa Borussia Dortmund, Michael Zorc amesema anaweza kumuona straika wa kimataifa wa Norway, Erling Braut Haaland katika klabu hiyo "kwa muda mrefu". Nyota huyo mwenye umri wa miaka 20 mkataba wake na miamba hao wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, unamalizika mwaka 2024. ***(Bild Sport)***

### AONGEZA MKATABA

MLINZI wa kushoto wa Argentina, Nicolas Tagliafico, ambaye amekuwa akihusishwa na Chelsea na Manchester City, amekubali kuongeza mkataba na Ajax ambapo sasa nyota huyo mwenye umri wa miaka 28 anatarajia kukaa na klabu hiyo ya Uholanzi hadi mwishoni mwa msimu. ***(De Telegraaf)***

### ALEXANDER-ARNOLD, RATIBA

MLINZI wa kulia wa Liverpool na England, Trent Alexander-Arnold mwenye umri wa miaka 22, amesema ratiba za michezo ya msimu huu inahitaji "akili ya kawaida". ***(Evening Standard)***

### KLABU ZA EPL NA MASHABIKI

KLABU za Ligi Kuu ya England zimeambiwa kupunguza idadi ya mashabiki kwenye viwanja hadi 1,000. ***(Telegraph)***

### KANA AIONA LIVERPOOL

MLINZI wa kati wa Anderlecht ya Ubelgiji, Marco Kana, mwenye umri wa miaka 18, amesema Liverpool ipo kwenye ndoto zake. ***(Walfoot, via Liverpool Echo)***

### BETTINELLI AWANIWA

GOLIKIPA wa Fulham, Marcus Bettinelli, mwenye umri wa miaka 28, anawaniwa na klabu kadhaa za Ligi Kuu ya England. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, ambaye anacheza kwa mkopo kule Middlesbrough, aliitwa kwenye kikosi cha England na kocha Gareth Southgate mwaka 2018. (Mail)

### MATEJ KUONDOKA BURNLEY

FOWADI wa Burnley raia wa Jamhuri ya Czech, Matej Vydra mwenye umri wa miaka 28, anataka kuondoka kwenye dimba la Turf Moor ili kutafuta timu atakayocheza mara kwa mara. ***(Accrington Observer)***

### GOMES ALIIKATAA MAN UTD

WINGA wa Uingereza, Angel Gomes mwenye umri wa miaka 20, amesema alikataa ofa ya Manchester United ili kujiunga na Lille kipindi cha majira ya joto. ***(Independent)***

### THAUVIN ATAJWA MILAN

MKURUGENZI wa ufundi wa AC Milan, Paolo Maldini, amekubali kwamba wanamuwania winga wa Ufaransa, Florian Thauvin mwenye umri wa miaka 27, ambaye mkataba wake na Marseille unamalizika kipindi cha majira ya joto cha 2021. ***(Telefoot)***

## HABARI MICHEZO

# KMC yajipanga kuvuna pointi tatu Dodoma

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa KMC FC, Habib Kondo, amesema kusongezwa mbele kwa michezo yao miwili, dhidi ya Namungo FC na Simba, hakutaathiri mipango yake na kumempa muda wa kujiandaa vizuri zaidi kwa ajili ya mechi yao dhidi ya Dodoma Desemba 4.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Kondo alisema baada ya kumalizana na Azam FC walitakiwa kucheza dhidi ya Namungo na baadae kucheza dhidi ya Simba, lakini mechi hizo zimesogezwa mbele kwa sababu timu hizo zinawakilisha nchi kwenye michuano ya kimataifa.

Alisema baada ya kusongezwa mbele kwa mechi hizo, amepata muda mwingi wa kuandaa kikosi chake pamoja na baadhi ya majeruhi kurejea kuwa fiti.

"Nina imani tutakuwa bora zaidi baada ya kufanyia kazi upungufu wa kikosi changu na sasa naendelea kujiandaa kuhakikisha tunapata pointi tatu muhimu katika mechi yetu hiyo dhidi ya Dodoma," alisema Kondo.

Alisema anawaheshimu wapinzani wao, lakini wachezaji wake wapo fiti tayari kupambana kutafuta matokeo mazuri katika mechi huo.

KMC inashuka dimbani ikiwa na kumbukumbu nzuri ya kuvuna pointi tatu katika mechi iliyopita dhidi ya Azam.

# Ushindi wapandisha molari Gwambina

**Na Saada Akida**

MATOKEO ya kushinda mechi mbili ugenini yamempa jeuri Kocha Mkuu wa Gwambina FC, Fulgence Novatus kwa kusema vijana wake wako tayari kuchukua pointi tatu kwa Namungo FC, Desemba Mosi, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti jana wakiwa safarini, Fulgence alisema matokeo ya kushinda mechi za ugenini yamewapa hamasa na kujiamini kwa wachezaji wake kupata matokeo mazuri katika mechi hiyo ya ugenini.

Alisema katika mechi tatu walizocheza wameshinda mbili dhidi ya JKT Tanzania na Mwadui na moja kutoka sare dhidi ya Yanga.

"Hatuwadharau wapinzani wetu, wako vizuri ndio maana wanawakilisha nchini kwenye mashindano ya kimataifa, lakini kwa matokeo ya mechi tatu wachezaji wamekuwa na ari ya kwenda kupambana kutafuta pointi," alisema Fulgence.

Alisema pia wana waheshimu Namungo timu nzuri pia imebadilisha kocha, hivyo ana imani itakuwa mechi ya ushindani mkubwa.

Gwambina watakuwa ugenini katika mchezo huo dhidi ya Namungo utakaopigwa Desemba Mosi mwaka huu uwanja wa Majaliwa, Ruwanga mkoani Lindi.

# ZAHERA ATAJWA AZAM

**Na Saada Akida**

ALIYEKUWA Kocha Mkuu wa Yanga, Mwinyi Zahera (pichani), ametajwa kuwa miongoni mwa walimu wanaopewa nafasi ya kurithi mikoba ya Aristica Cioaba kule Azam FC.

**Azam ilimtimua kocha wake, Cioaba baada ya kufungwa na Yanga bao 1-0, huku uongozi wa timu hiyo ukisema sababu ni kutokana na matokeo mabaya ya mechi tatu za timu hiyo kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.**

Taarifa za uhakika zilizoifikia gazeti hili kutoka ndani ya klabu hiyo, zinasema kwamba, Zahera amependekezwa kukabidhiwa majukumu ya kukinoa kikosi hicho.

Mtoa habari huyo alisema uamuzi wa kuondolewa Cioaba ulifanyika usiku baada ya mechi dhidi ya Yanga, pia muda mfupi likapendekezwa jina la Zahera.

"Hadi sasa Zahera ndio amekuwa chaguo la kwanza, mwenyewe mmiliki wa timu (bosi), ndio alipendekeza jina la kocha huyo, hivyo tunasubiri kama kutakuwa na mabadiliko zaidi ya hayo," alisema mtoa habari huyo.

Alipotafutwa Mtendaji Mkuu wa timu hiyo, Abdukarim Amin 'Popat' kuzungumza suala la kocha alisema, "Kwa Sasa sitaweza kuzungumza lolote naomba umtafute msemaji wetu, Zakaria Thabit."



Gazeti hili lilipomtafuta msemaji huyo, alisema kwamba kuna taarifa zimekuwa zikizungumzwa muda mrefu tangu kipindi ambacho Azam walivyomuondoa Hans Pluijm.

"Kuhusu Zahera ni taarifa za muda mrefu, pia sio rahisi, kwanza huyo kocha anafanya kazi sehemu nyingine, kwa sasa timu ipo chini ya Vivier Bahati hadi hapo kocha mkuu atakapopatikana," alisema Zakaria.

Alisema kwa sasa timu hiyo inasimamiwa na kocha huyo msaidizi huku mchakato wa kutafuta mrithi wa Cioaba ukiendelea baada ya kuanza kupokea CV kwa walimu kutoka mataifa mbalimbali.




Mchezaji wa Yanga Princess, Aniella Uwimana (kushoto), akimiliki mpira huku akizongwa na mchezaji wa Tanzanite, Joyce Lema, katika mchezo wa Ligi Kuu ya Soka la Wanawake uliochezwa Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Kocha ataja sababu Chuoni kuanza vibaya*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA wa timu ya Chuoni, Ali Bakar Mganzija, amesema kuanza vibaya kwa timu yake katika ligi kuu ya Zanzibar ni kutokaa na mabadiliko ya mchezo uwanjani, ambayo yanatokea.

Chuoni tayari imecheza michezo miwili ambapo mchezo wake wa kwanza ilifungwa 1-0 na Malindi na mchezo wake wa juzi, ilitoka sare ya 1-1 dhidi ya Black Sailor iliyopanda daraja msimu huu.

Akizungumza na gazeti hili, kuhusu michezo hiyo miwili Mganzija alisema haoni kama wachezaji wake wanatatizo, lakini ni mabadiliko ya mchezo wenyewe, kwani timu huwa zinataka kupata ushindi katika mechi za mwanzo wa ligi.

Alisema mchezo wao wa kwanza wachezaji walicheza vizuri na walipambana, lakini wapinzani wao walitumia vizuri nafasi waliyoipata na wakafungwa.

Alisema katika mchezo wa juzi dhidi ya Black Sailor, timu hiyo ilicheza vizuri na kupoteza nafasi nyingi za wazi.

"Mwanzo wa ligi kila timu inahitaji kufanya vizuri mapema, hivyo mchezo lazima uwe wa ushindani wa hali ya juu na ndio maana wachezaji wakiwa uwanjani wanaangalia zaidi kufunga," alisema.

# Michezo

Jumapili Novemba 29, 2020

Nipashe




Ni Lampard vs Mourinho leo UKURASA 22



Kiungo wa Yanga, Deus Kaseke (katikati), akipiga mpira kufunga bao dhidi ya JKT Tanzania, katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania bara uliopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# YANGA INA JAMBO LAKE MSIMU HUU

## ●●● Yaendelea kuangusha moja moja Ligi Kuu...

**Adam Fungamwango**

MCHEZAJI Deus Kaseke, kwa mara nyingine tena ameendelea kuwa shujaa wa timu ya Yanga, baada ya kufunga bao pekee lililoipa timu hiyo ushindi wa bao 1-0 dhidi ya JKT Tanzania na kutwaa pointi tatu muhimu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam, ikiendelea kujikita kileleni mwa Ligi Kuu Tanzania Bara.

**Jumatano iliyopita, Kaseke alifunga bao pekee dhidi ya Azam FC kwenye Uwanja wa Azam Complex ikiipa Yanga pia ushindi wa bao 1-0.**

Mchezaji huyo ameipa timu yake pointi sita muhimu kwenye kinyang'anyiro cha kusaka ubingwa wa Tanzania Bara msimu huu.

Straika raia wa Burkina Faso, Yacouba Songne ambaye alitoa pasi kwa Kaseke kwenye mechi iliyopita, ndiye pia aliyetoa pasi jana iliyomkuta Kaseke na kuujaza wavuni dakika ya 32.

Bao hilo lilipatikana baada ya wachezaji wa Yanga kukosa mabao mengi ya wazi na kuanza kuwatia presha mashabiki wa timu hiyo.

Kosa kosa kwenye mechi hiyo zilianza dakika ya tisa, kipa wa Yanga Metacha Mnata alifanya kazi ya ziada baada ya kupangua shuti kali lililopigwa na Shaaban Mgandila nje kidogo ya eneo la hatari na kuwa kona ambayo haikuleta madhara.

Yanga ilikosa nafasi ya wazi ya kuandika bao dakika ya 13, baada ya kutokea kizaazaa kwenye lango la JKT Tanzania, lakini kina Nchimbi, Yocouba Songne na Deus Kaseke walishindwa kuuweka mpira uliokuwa unazagaa wenyewe ndani ya nyavu.

Nchimbi alikosa bao la wazi zaidi ambalo ilikuwa vigumu kukosa kuliko kupata dakika ya 25, alipobaki yeye na kipa wa JKT Tanzania, Joseph Ilunda, lakini alichofanya badala ya kupiga ni kumpasia tu mikononi.

Dakika ya 32, ndipo Kaseke aliposhusha presha ya mashabiki wa Yanga uwanjani hapo alipoipatia timu yake bao la kwanza akiwa katikati ya mabeki wa JKT Tanzania, baada ya pasi ya kuchomokewa kutoka kwa Yacouba.

Nusura JKT Tanzania isawazishe bao dakika ya 41, baada ya straika wake hatari, Adam Adam alipogeuka ghafla akiwa na mpira, akiachia shuti kali lililopaa juu kidogo ya lango.

JKT Tanzania ilikosa nafasi nyingine ya kusawazisha bao dakika ya 45, Michael Aidan akipiga shuti la mbali lililotemwa na kipa Metacha, lakini Daniel Lyanga alishindwa kuuwahi, kabla ya kipa huyo kuuwahi tena na kuisalimisha timu yake.

Kipindi cha pili hakukuwa na mashambulizi sana ya hatari, ingawa JKT Tanzania ilionekana kuamka na kufanya mashabulizi kupitia kwa Abdallah Shaibu 'Ninja' aliyeingia badala ya Paul Godfrey, lakini washambuliaji wake kina Adam, Mgandila na Lyanga walikuwa wakijichanganya wenyewe.

Kwa matokeo hayo, Yanga inafikisha pointi 31, ikiwa kileleni, ikicheza mechi 13, huku JKT Tanzania ikiwa kwenye nafasi ya 16 juu ya Mbeya City na Ihefu, kwa pointi 10 tu ilizonazo, ikicheza pia mechi 13 mpaka sasa.

# Simba yatupa karata ya kwanza kimataifa

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA wa Tanzania Bara, leo wanaanza safari yao ya mechi za kimataifa, itakapocheza dhidi ya Plateau FC ya Nigeria kwenye Uwanja wa New Jos uliopo nchini humo.

Mechi hiyo inayotarajiwa kuanza saa 10:00 jioni kwa saa za Nigeria, Tanzania ikiwa ni saa 12:00 jioni, ni ya raundi ya awali ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa ajili ya kusaka bingwa wa msimu huu.

Ni mechi ambayo inatarajia kutoa dira ya soka la Tanzania kama ikifanya vema itakusanya pointi ambazo zinaweza kusaidia msimu ujao kuongezwa kwa timu za kucheza michuano ya kimataifa kutoka mbili hadi kufikia nne, kama ilivyokuwa mwaka jana.

Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck, amesema kuwa mechi itakuwa ngumu kutokana na wenyeji kutaka kushinda ili kujiweka katika mazingira mazuri kwa mechi ya marudiano, lakini na wao pia wamejipanga kwa ajili ya kupata ushindi pia.

"Hatuchezi ili kuzuia tusifungwe, ina tunacheza kwa ajili ya kusaka ushindi. Tunakata kushinda mechi ya ugenini ili tujiweke vizuri kwenye mechi ya marudiano ambayo tunacheza mbele ya mashabiki wetu, tucheze bila presha," alisema kocha huyo.

Iwapo Simba itafanikiwa kupita kwenye hatua hii, itakumbana na mshindi kati ya FC Platinumz ya Zimbabwe dhidi ya Costa do Sol ya Msumbiji.

Simba inaingia kwenye mechi ya leo ikiwa na kumbukumbu ya kutolewa mapema kwenye michuano hiyo msimu uliopita dhidi ya UD Songo ya Msumbiji.

Kwenye mechi ya kwanza ugenini ilitoka sare ya bila kufungana, huku ikilazimishwa sare ya bao 1-1 na kutolewa kwa goli la ugenini.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >